# Nipashe

Jumanne Juni 30, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580271

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




MAHOJIANO MAALUM

## Zitto Kabwe auweka kiporo uamuzi wake kujitosa urais

UKURASA 4

# Kipenga urais, ubunge CHADEMA chapulizwa

• **Ratiba** yote hadharani, mpeperusha bendera urais kujulikana...*Endelea ukurasa 2*



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Atlas, eneo la Madale, jijini Dar es Salaam, wakipimwa joto la mwili ikiwa ni sehemu ya kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona, kabla ya kuingia madarasani, baada ya shule kufunguliwa jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



**BAA LA CORONA**

**Jambo muhimu la kuzingatia kuhusu virusi vya corona vinapokuwa kwenye hewa ni kwamba vinaweza kuepukwa kwa kupuliza dawa zin-azotumika nyumbani. WHO**

- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Wanafunzi warejea, tahadhari ya corona yawekwa

UKURASA 3



## Magufuli afichua viongozi serikalini, CCM wachochea migogoro ya ardhi

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO YANGA, KAGERA MECHI YA KISASI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA




Rais John Magufuli akiwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe na viongozi mbalimbali akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa mahandaki ya reli ya kisasa (SGR) katika eneo la Kilosa mkoani Morogoro, jana. **PICHA: IKULU**

# Kipenga urais, ubunge CHADEMA chapulizwa

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetangaza mchakato wa uchukuaji fomu za urais, ubunge na udiwani upande wa Tanzania Bara.

Kimesema mchakato huo unatarajiwa kuanza rasmi Julai 4 mwaka huu kwa wagombea urais kuanza kuchukua, kujaza na kutafuta wadhamini hadi Julai 19 mwaka huu.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa CHADEMA, Reginald Munisi, alitangaza kuanza kwa mchakato huo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana.

Alisema kuanzia Julai 4, yaani Jumamosi, wagombea urais wataanza kuchukua fomu za kuwania nafasi mbalimbali wao wenyewe au kutuma mawakala wao katika ofisi ya Katibu Mkuu Bara.

Alisema kila mgombea atakuwa na nafasi ya kujaza fomu na kutafuta udhamini katika kanda 10 zikiwamo nane za Tanzania Bara na mbili za Zanzibar.

"Kwenye kila kanda, mgombea anatakiwa kupata wadhamini wasiopungua 100 na kutakuwa na maofisa wa chama watakaokuwa wanawapatia maelekezo ya namna ya kujaza fomu hizo," alisema.

Kuhusu mdhamini, Munisi alisema hatakiwi kuwa mjumbe wa mkutano mkuu wa CHADEMA ambao ndiyo utapitisha jina la mgombea katika hatua za mwisho za mchakato huo.

Munisi alisema Julai 19, itakuwa mwisho wa kuchukua fomu, kujaza, kutafuta wadhamini na kuzirejesha makao makuu ya chama.

Alisema Julai 22, Katibu Mkuu wa CHADEMA atawasilisha taarifa za watia nia katika mkutano wa kamati kuu ili ipendekeze wanaofaa kuingia katika hatua inayofuata.

Munisi alisema kuwa Julai 28, Baraza Kuu litakaa na kuchuja majina na baada ya hapo yatachekechwa na kupelekwa mkutano mkuu ambao utakaa Julai 29 na kupitisha jina la mgombea urais.

**WABUNGE**

Kuhusu mchakato wa wagombea nafasi ya ubunge, Munisi alisema fomu zitaanza kutolewa Julai 4 katika ofisi za majimbo na zitapatikana pia kwenye tovuti ya chama.

"Wagombea wote wanapaswa kuchukua fomu, kuzijaza na kuzirejesha kwa jimbo wanalogombea au wilaya kwa hatua zinazofuata na mwisho utakuwa Julai 10 saa 10:00 jioni," alisema.

Munisi alisema baada ya hapo hatua mbili zitafuata katika majimbo ikiwamo wagombea wote kuitwa na kamati za utendaji za jimbo na kuwahoji kuhusu sifa zao, uanachama wao, uadilifu wao na maono yao na watatoa alama kwa njia ya kujaza fomu.

Alisema hatua ya pili wataangalia kuhusu kukubalika kwa mtia nia husika katika nafasi ya ubunge, lakini hawataruhusiwa kukata jina kwa kuwa majina yote yataenda kwenye kura za maoni katika mkutano mkuu wa jimbo.

Alisema kura za maoni zitatoa mwelekeo wa nani anafaa kupeperusha bendera ya chama na baada ya kikao hicho, kamati ya utendaji itakaa tena kupendekeza na kufanya uteuzi wa awali.

"Watafanya mapendekezo ya awali ya nani ateuliwe kupeperusha bendera ya chama na mchakato wote huu utasimamiwa na uongozi wa kanda," alisema.

Munisi alisema kuwa baada ya hapo, kamati ya utendaji ya kanda itakaa na kutoa maoni ya kwa kila mgombea na watawasilisha taarifa kwa Katibu Mkuu wa Chadema ambaye atawasilisha taarifa kwa kamati kuu ya chama ambayo itapitia mapendekezo yote na kuteua mgombea.

"Julai 30 hadi 31, kamati kuu itakaa kwa ajili ya kupitisha majina ya wagombea wa nafasi hizo katika majimbo yote nchini," alibainisha.

**MADIWANI**

Kuhusu mchakato wa madiwani, Munisi alisema fomu zitapatikana katika ofisi za kata, majimbo na tovuti ya chama.

Alisema kuanzia Julai 11 hadi 17 ni muda wa kuchukua na kurudisha fomu za kuwania nafasi ya udiwani na hatua nyingine zitafuta ikiwamo kuhojiwa na kamati ya utendaji ya kata ambayo itawapatia maksi.

Baada ya hapo watapigiwa kura ya maoni na kamati ya utendaji ya kata kuanzia Julai 20 hadi 23.

"Hizi zinachelewa kidogo ili mtu akiona nafasi ya ubunge haijaenda vizuri, aweze kuomba udiwani ili tusijepoteza watu ambao wana uwezo mzuri tu, anaweza asitoshe kwenye ubunge akatosha kwenye udiwani," alifafanua.

Munisi aliongeza kuwa Julai 24, kamati ya utendaji za majimbo yote nchini, zitateua majina ya madiwani wa kupeperusha bendera ya CHADEMA.

**VITI MAALUM**

Kuhusu mchakato wa viti maalum, Munisi alisema uko kwenye mwongozo wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) na ratiba yao iko kama ya wagombea wa majimbo.

Alisema wakati mkutano mkuu wa chama kanda ukipiga kura za maoni za wagombea, BAWACHA nao watapiga kura za maoni za viti maalum.

Alisema hadi kufika Septemba 25, watakuwa washapitisha majina ya Viti Maalum wa CHADEMA.

"Niwakumbushe Watanzania wote umuhimu wa zoezi tunaloenda kulifanya, maana ya uhuru, maana ya kujitawala ni kuweza kuamua ni nani sisi tunamtaka na siyo mtu mwingine atuamulie," alisema.

Aliwakaribisha wanachama wote wa CHADEMA wenye sifa na nia ya kuwania nafasi mbalimbali kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, kujitokeza kuchukua fomu kuwania nafasi hizo.

## JPM afichua viongozi serikalini, CCM wachochea migogoro ardhi

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli amesema migororo ya ardhi katika mikoa ya Morogoro na Pwani inachochewa na baadhi ya viongozi ndani ya serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alitoa kauli hiyo jana wilayani Kilosa mkoani Morogoro wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika mahandaki ya reli ya kisasa(SGR) kutoka Morogoro hadi Makutupora.

"Kuna baadhi ya viongozi walioko ndani ya serikali wanahusika na migogoro hii, nimeshapata habari hata viongozi wa chama changu, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya (ya Kilosa), analaumiwa kwa kuhusika na migogoro hii, na mimi ni msema kweli, msema kweli ni mpenzi wa Mungu," alisema.

Rais Magufuli aliongeza akionya: "Sasa niwaombe viongozi wote wanaohusishwa na migogoro ya mashamba, muitatue kwa kumtanguliza Mungu mbele, siwezi nikawa na taifa la Watanzania milioni 60, wanakosa mahali pa kulima.

"Nimeambiwa kuna eneo amepewa mwekezaji wala siyo Mtanzania. Hebu Watanzania mjiulize mkienda kutafuta ardhi kwenye maeneo yao hao, mtapata hata ekari moja?"

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, Sheria ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007, na hata Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995, ardhi ya Tanzania atamilikishwa Mtanzania peke yake.

"Akipatikana mtu ambaye siyo Mtanzania na anataka kumiliki hiyo ardhi, lazima aende Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), akapewe kibali na mkataba maalum wa kuiendesha na kwa masharti maalum.

"Na kwa mujibu wa sheria hiyo hiyo, unapopewa ardhi, ni lazima uiendeleze, lakini watu wamechukua maeneo na hawayaendelezi, kuanzia Pwani hadi Morogoro," alisema.

Rais Magufuli alimwagiza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, kuunda tume ambayo itafanyia kazi migogoro ya ardhi katika maeneo hayo. Pia, aliagiza Waziri wa Mambo ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, kuwa sehemu ya tume itakayoundwa.

"Ninataka ndani ya siku saba, yale mashamba yaliyobaki nayo tuyafute, lakini ninataka mpange mikakati ya namna ya kuwagawia wananchi maskini," aliagiza.

Rais aliwaomba viongozi wa dini kusaidia katika kutatua migogoro hiyo, huku akizitaka mamlaka kutowaonea watu ambao wanamiliki mashamba na wameyaendeleza.

"Lakini niwaombe viongozi, wasiwaonee watu wengine ambao wana mashamba yao na wameyaendeleza, lisije hili agizo likatafsiriwa kwamba sasa ni kwenda kuchukua mashamba ya watu.

"Wapo walio na mashamba yao na wameyaendeleza, nina uhakika mkipanga vizuri matumizi ya ardhi na mkashirikisha viongozi mpaka kwenye ngazi za vijiji, tutatatua hili tatizo," alifafanua.

Rais Magufuli aliagiza kuundwa kwa tume hiyo baada ya kutangaza kuwa tayari ameshafuta umiliki wa mashamba 46 na mengine yanasubiri uamuzi ambao aliahidi kuutoa kabla ya Jumamosi.

**DC, DED WAONYWA**

Kiongozi huyo wa nchi pia aliwaonya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilosa na Mkuu wa Wilaya hiyo kwa kushindwa kutatua kero za wananchi wa eneo hilo pamoja na kudaiwa kuhusika katika kashfa mbalimbali.

"Nimeambiwa mkurugenzi wa hapa naye ana matatizo, ajirekebishe, siwezi nikamtumbua mbele ya askofu, madhambi yake anayajua, ameuza eneo na alifanya kikao siku hiyo hiyo na mkataba akasaini siku hiyo hiyo.

"DC (Mkuu wa Wilaya) wa Kilosa na wewe jirekebishe, sitaki kuwaficha ndugu zangu, taarifa ninazo za kutosha, ninasikia unaenda na polisi kwenda kuwazuia wananchi wasiingie kwenye shamba, badala ya kuwatetea wananchi unatetea ambao hata huwajui," alionya.

# Shule zafunguliwa, tahadhari dhidi ya corona yachukuliwa

**Na Waandishi wetu**

JANA wanafunzi wa shule za awali hadi kidato cha nne walirejea shuleni baada ya kupumzika tangu Machi 18, mwaka huu, kutokana na janga la corona.

Wanafunzi hao wamerejea baada ya Rais John Magufuli kutangaza kufunguliwa kwa shule hizo, huku Wizara za Elimu na Afya zikitoa mwongozo wa namna ya kuendelea na masomo kwa kuchukua tahadhari ya corona.

Katika shule wanafunzi walizorejea jijini Dar es Salaam na Dodoma, kulikuwa na maji ya kunawa mikono na kila mwanafunzi kuvaa barakoa isipokuwa wenye matatizo ya kiafya au chini ya miaka nane.

Aidha, katika shule nyingi wanafunzi walionekana wakiwa wamevaa barakoa, huku walimu na wafanyakazi wengine wakichukua tahadhari.

Baadhi ya wanafunzi walirudishwa nyumbani kwa kukosa barakoa, jambo ambalo liliwafanya wakose masomo kwa siku ya jana.

Pia, baadhi ya wazazi wamelalamikia mchanganuo wa kulipa ada kwa robo ya pili huku baadhi ya shule zikiwataka kulipa fedha ya chakula na usafiri kwa ukamilifu wake.

**Mambo mengine ambayo wazazi walilalamikia ni kitendo cha shule kufunguliwa na kutangaziwa waanze kuwapeleka watoto Jumapili, lakini mazingira ya shule wameyakuta machafu, huku uongozi ukipaka rangi mabweni siku hiyo.**

Wazazi wa wanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Atlas iliyopo Madale jijini Dar es Salaam, wamewasilisha malalamiko yao kwa uongozi ikiwamo mchanganuo wa ulipaji ada wa kumalizia robo ya kwanza ya muhula wa pili.

Vilevile wamewasilisha malalamiko kuhusu hali ya mazingira ya shule hiyo na taratibu nyingine zinazotumika.

Mapendekezo hayo yalipokelewa juzi jioni na Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Joseph Msafiri, ambaye alifafanua kuwa suala la ulipaji wa ada kwa muhula wa kwanza wazazi halipingiki kutekelezwa na wazazi wote kwa sababu serikali umeusogeza.

Kuhusu muhula wa pili kwa robo ya kwanza, alisema yapo mazungumzo yanayoendelea kwenye uongozi wa shule ili kutoa nafuu kwa wazazi wa wanafunzi wa darasa la saba.

Mambo mengine ambayo wazazi walilalamikia ni kitendo cha shule kufunguliwa na kutangaziwa waanze kuwapeleka watoto Jumapili, lakini mazingira ya shule wameyakuta machafu, huku uongozi ukipaka rangi mabweni siku hiyo.

Akitolea ufafanuzi wa changamoto hiyo, Msafiri alikiri wamewapokea watoto huku shule ikiwa na mazingira machafu na hiyo imetokana na ukosefu wa fedha.

Msafiri alikiri changamoto ya watoto kutopewa maji ya kunywa wakati mwingine na kufafanua kuwa husababishwa pale panapotokea tatizo la huduma hiyo.

Katika hilo wazazi walilalamikia uongozi kuwa licha ya wao kutozwa fedha za kujikimu 'pocket money', lakini inapotokea changamoto hazitumiki hata kununua maji ya watoto.

**DODOMA**

Katika Shule ya Msingi Makole, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Veronica Mrope, alisema: "Ili kuwaondolea hofu wanafunzi na walimu, kabla ya kuanza masomo wanafanya maombi ili kuwalinda katika masomo yao."

Nipashe pia ilitembelea, Shule ya Sekondari Dodoma na Central kuangalia mwenendo wa mitihani ya kidato cha sita iliyoanza jana nchini na kushuhudia ulinzi ukiwa umeimarishwa na tahadhari za ugonjwa huo zikiwa zimezingatiwa.

Aidha, baadhi ya shule zimechukua tahadhari kwa kuweka vifaa vya kunawa mikono kwenye maeneo yote muhimu ya kuingia na kuzingatia uvaaji wa barakoa.

Katika Shule ya Sekondari Dodoma, Viwandani, Shule ya Msingi Mlimwa C, Kiwanja cha Ndege na Fountain Gate Academy, wanafunzi walionekana wakiingia kwa mpangilio huku wakipimwa joto na kunawa mikono.

Pamoja na mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huo, baadhi ya shule zimeongeza muda wa masomo ili kumaliza muhtasari ya mihula inavyotakiwa.

Mkuu wa Shule ya Dodoma Sekondari, Amani Mfaume, alisema wamejipanga kufundisha hadi siku za Jumamosi kwa baadhi ya vidato ili kufidia muda wa kumaliza muhtasari waliyotakiwa kufundisha.

Naye, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Fountain Gate Academy, Abilius Wamara, alisema shule imeongeza saa mbili ili kumaliza mihula kwa muda uliopangwa.

Aidha, alisema pia wamechukua tahadhari zote za kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo kuwatakasa mikono wanafunzi kabla ya kupanda gari la shule na kupimwa joto na kunawa mikono kabla ya kuingia eneo la shule.

Katika hatua nyingine, Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege na Mlimwa C, baadhi ya wanafunzi wasiokuwa na barakoa walirudishwa nyumbani ili kuvaa.

Mmoja wa wanafunzi, AbdulMarik Juma, ambaye anasoma Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege, alionekana akirudi nyumbani baada ya kufika shule na alipoulizwa, alisema amekatazwa kuingia shule kwa kuwa hajavaa barakoa.

"Nimerudishwa nyumbani na mwalimu kaniambia hairuhusiwi kuingi darasani bila kuvaa barakoa," alisema.

Naye, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mlimwa C, Merina John, alisema amezuiliwa kuingia shule kwa kuwa hana barakoa.

Ofisa Elimu wa Shule za Msingi, Joseph Mabeyo, alisema hawezi kuzungumzia suala hilo hadi mwandishi apewe kibali na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

***Imeandikwa na Romana Mallya (DAR), Ibrahim Joseph na Renatha Msungu, Peter Mkwavila na Paul Mabeja (DODOMA)***

# Mwakilishi ajiengua mbio za urais Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKILISHI wa Jimbo la Mtoni Ibrahim Makungu ambaye ni miongoni mwa wanachama 32 wa CCM waliochukua fomu ya kugombea urais wa Zanzibar amejitoa katika kinyang'anyiro hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, alisema ameamua kufanya hivyo kutokana na baadhi ya wagombea waliojitokeza kuwa na uwezo mkubwa na sifa kuliko yeye.

Alisema pia sababu nyingine ya kujiengua katika kinyang'anyiro hicho ni wananchi wa Jimbo la Mtoni bado wanamuhitaji katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

Alieleza kuwa uamuzi wake huo utakirahisishia chama kufanya kazi zake katika kujadili wagombea hao katika vikao vyake mbalimbali.

"Kwa sasa nitaendelea kushiriki kugombea nafasi ya uwakilishi katika jimbo langu kwani bado wananchi wananihitaji, na nimeshajipanga vizuri kuhakikisha nawawekea mazingira mazuri wanafunzi hasa wa usafiri," alisema.

Ibrahim alieleza kuwa hajashawishiwa na mtu yeyote kujitoa katika kinyang'anyiro hicho bali ni uamuzi wake katika kupunguza muda katika kujadili wagombea katika vikao vinavyotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Alisema atahakikisha anashirikiana na mgombea urais atakayeteuliwa na chama katika kukipatia ushindi chama hicho katika uchaguzi mkuu.

Katika hatua nyingine idadi ya wagombea waliorejesha fomu imefikia 24 ambapo jana wagombea watano walirejesha akiwamo Jecha Salum Jecha, Perera Ame Silima, Bakar Rashid Bakar, Hasna Attai Masoud na Mussa Aboud Jumbe.

Akizungumza baada ya kurejesha fomu hiyo Hasna Attai Masoud alisema anasubiri maamuzi ya chama na kuwataka wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi badala ya kusubiri nafasi za kuteuliwa.

Wagombea 32 waliochukua fomu ni Mbwana Bakari, Balozi Ali Karume, Mbwana Mwinyi Yahya, Omar Shehe, Muhammed Jafar, Muhammed Hija, Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor, Shamsi Vuai Nahodha na Dk. Hussein Mwinyi.

Wengine ni Profesa Makame Mbarawa, Mwatum Mussa Sultan, Haji Rashid Pandu na Dk. Abdul-halim Mohammed Ali, Jecha Salim Jecha na Dk. Khalid Salum Muhamed.

Wengine ni Rashid Ali Juma, Khamis Mussa, Mmanga Mjengo Mjawiri, Hamad Yussuf Masauni, Muhammed Aboud, Bakari Rahid, Ibrahim Makungu, Ayoub Muhammed Mahmoud, Hashim Salum Hashim na Hasna Ataai Maoud.

Wamo pia Fatma Kombo Masoud, Pereira Ame Silima, Iddi Hamad Iddi, Shaame Ame Silima, Mussa Aboud Jumbe, Mgeni Hassan Juma na Maudline Castico.


ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

Jengo la EWURA, Medeli Magaharibi
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

**NOTISI YA KUSUDIO LA KUFUTA LESENI ZA UENDESHAJI BIASHARA YA MAFUTA YA PETROLI KWA JUMLA**

**(Imetolewa chini ya Kanuni ya. 21 (2) ya Kanuni za Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) Rules, Toleo la Gazeti la Serikali Na. 380 la 2018)**

**NOTISI** ya siku ishirini na moja (21) inatolewa kwa makampuni yafuatayo kuwa EWURA inakusudia kufuta leseni zao za uendeshaji biashara ya mafuta ya Petroli kwa kushindwa kufanya biashara ya mafuta kwa jumla kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita kinyume na masharti ya leseni na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) Rules, Toleo la Gazeti la Serikali Na. 380 la 2018.

Endapo kampuni hizo hazitawasilisha sababu zinazokubalika na kujitosheleza kisheria kwa nini leseni zao za uendeshaji wa biashara ya mafuta ya petrol kwa jumla zisifutwe, EWURA itaendelea na utaratibu wa kufuta leseni hizo baada ya kuisha kwa siku ishirini na moja toka tarehe ya notisi hii pasipo notisi nyingine. Makampuni ambayo EWURA inakusudia kufuta leseni zao ni:

1. **Jina la Kampuni:** Alser Limited
   **Nambari ya Leseni:** PWL-2017-001
   **Anwani ya Ofisi:** Kiwanja Na. 7/8, Mtaa wa Ghana/ Ohio, Manispaa ya Ilala
2. **Jina la Kampuni:** Enoc Africa Limited
   **Nambari ya Leseni:** PWL-2016-013
   **Anwani ya Ofisi:** Kiwanja Na. 424, Toure Drive, Maeneo ya Oyster Kinondoni
3. **Jina la Kampuni:** Express Oil Limited
   **Nambari ya Leseni:** PWL-2016-015
   **Anwani ya Ofisi:** Kiwanja Na. 66, Kitalu "F", Mtaa wa Kikale, Manispaa ya Temeke
4. **Jina la Kampuni:** Apex Energy Limited
   **Nambari ya Leseni:** PWL-2016-010
   **Anwani ya Ofisi:** Kiwanja Na. 14, Kitalu "C", Eneo la Tuangoma, Wilaya ya Kigamboni

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA,**

215792702

MAHOJIANO MAALUM

# Zitto Kabwe auweka kiporo uamuzi wake kujitosa urais

## ■ Aanika msimamo wa ACT kumpokea Membe
## ■ Inampa tabu TANAPA kukwama mishahara

**Na Enock Charles**

JOTO la siasa kuelekea uchaguzi mkuu na hasa wa urais, limepamba moto. Ndani ya Chama cha ACT-Wazalendo, nako hali hiyo imetawala, tetesi zikisambaa za Kiongozi Mkuu wa chama, Zitto Kabwe, kuchukua fomu kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano, vivyo hivyo, baadhi ya walio nje ya chama.

Kupata majibu bayana ya hayo, Nipashe ilimtafuta Zitto kupata kauli ya kinywani mwake, hali kadhalika ufafanuzi wa tetesi mbalimbali za uchaguzi na nyinginezo za kisiasa ambazo sasa ndiyo zimetawala jikoni. Zitto ana haya katika ufafanuzi wake:

...

***SWALI: Kuna tetesi kwamba awamu hii hautagombea ubunge na badala yake unafikiria kuwania urais. Kuna ukweli katika hili?***

**ZITTO:** Tetesi za kwamba sitagombea ubunge, ninagombea urais nizichukulie kama tetesi kwa sasa kwa sababu nilieleza hili kwenye mkutano wa viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Walileta maombi maalum ya kunitaka nitoe tamko la kwamba mwelekeo wangu wa kisiasa unakuwaje kwa sababu chama kinahitaji mtu ambaye atapeperusha bendera yake.

Niliwashukuru viongozi na wanachama wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa ombi lao ambalo walilitoa, lakini nikiwaambia kwamba lazima niende nikafanye mazungumzo na wapigakura wangu wa Jimbo la Kigoma Mjini, ili kukubaliana ni hatua gani sasa inayofuata kuhusiana na mwelekeo wa kisiasa.

Kwa hiyo, hili nitalijibu baada ya kumaliza ziara yangu na mashauriano na viongozi, wanachama, wananchi na wazee wa Mji wa Kigoma na Mkoa wa Kigoma pamoja na mkutano mkuu wa Mkoa wa Kigoma wa Chama cha ACT-Wazalendo ambao tutajadiliana hayo.

Ni lazima tuangalie maslahi mapana ya taifa, lakini vilevile kuangalia na maslahi ya Mkoa wa Kigoma kwa kuwa wao ndiyo wamenifanya niweze kufahamika nchi nzima.

***SWALI: Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe, ameweka wazi kwamba kuna makada wa CCM wanaofikiria kuwania urais kupitia upinzani. Je, ACT mmeshapata ombi lolote?***

**ZITTO:** Suala la Ndugu Benard Membe ninafikiri angepaswa kulizwa mwenyewe kwa sababu si mwanachama wetu, na kama kuna lolote ambalo linaweza likatokea, hilo ni jambo ambalo tunaweza tukalizungumza baadaye kwa pamoja. Sitaweza kulijibu kwa hatua ya sasa.

***SWALI: Siku moja kabla ya Bunge la 11 kuvunjwa, ulisimama bungeni na kuibua hoja ya kupinga uamuzi wa serikali kukusanya mapato ya mamlaka za kihifadhi kwa maana ya Ngorongoro na TANAPA na TAWA. Wewe ni mtaalamu wa uchumi, uamuzi huu una athari zipi kiuchumi?***

**ZITTO:** Kuhusiana na Mamlaka ya Mapato (TRA) kukusanya mapato ya Ngorongoro na TANAPA (Shirika la Hifadhi za Taifa) niliongea bungeni japo kwa kifupi sana, lakini kiufasaha zaidi ni kwamba, kwa sababu hizi ni mamlaka za uhifadhi, ni vizuri ziwe na uhuru wa kukusanya na kutumia mapato yao, ili kuhakikisha uhifadhi hauporomoki nchini.

Kwa hatua ambayo serikali imechukua kwa kuamua TRA kukusanya mapato haya, maana yake ni kwamba kutakuwa na hatari kubwa sana kwa siku za usoni uhifadhi kuporomoka.

Na hatari hii inaweza kusababisha ujangili kurudi, inaweza kusababisha utalii kuporomoka na hata miundombinu ya msingi katika hifadhi kutokupatiwa huduma inavyostahili na tayari tumeshaambiwa kwamba eeh TANAPA mwaka huu kwa miezi michache iliyopita wameshindwa kulipa mishahara kutokana na madhara ya corona.



Kama TANAPA wana akiba ya kutosha kwenye akaunti zake, mimi nikiwa mwenyekiti wa Kamati ya Bunge inayohusika na mashirika ya umma na baadaye serikali kuu, ninafahamu kwamba TANAPA walikuwa na akiba ya kutosha kabisa kwenye benki kuweza kuendeleza shughuli zao bila wasiwasi wowote hata kama wangekuwa hawana mapato kwa mwaka mzima.

Kitendo kilichotokea kwamba corona imetokea miezi michache tu na baadaye TANAPA hawana fedha ya kulipa mishahara, inaonyesha dhahiri kwamba serikali ilikuwa tayari imeshaanza kutumia fedha za TANAPA kinyume cha taratibu ambazo zipo.

Kwa hiyo, mimi ninadhani serikali kuchukua na kutaka TRA waanze kukusanya vyanzo hivi vya mapato ni tatizo na si sawa kwa mustakabali wa uhifadhi na utalii nchini.

***SWALI: Nini hasa kilisababisha ukamatwe na kushikiliwa kwa siku mbili na Jeshi la Polisi wilayani Kilwa wiki iliyopita?***

**ZITTO:** Kama inavyofahamika kwamba sisi tulikuwa na ziara ambayo ilianzia Mkoa wa Pwani katika Wilaya ya Rufiji ambako tulipokea wanachama walikuwa ni madiwani wa vyama vingine takriban wanne katika jumla ya madiwani sita waliotoka upinzani katika Jimbo la Rufiji na siku ya pili tulikuwa tunafanya kazi Kilwa na tulikuwa tumeshaanza kikao chetu cha ndani kwa ajili ya kupokea wanachama wengine wakiwamo madiwani.

Cha kushangaza askari wa Jeshi la Polisi, wakiongozwa na OCD wa Kilwa, Ndugu Banzi, walivamia mkutano ule na kunikamata kwa nguvu pamoja na viongozi wenzangu wanane ambao wote tulipelekwa Kituo cha Polisi Kilwa, tukakaa pale kuanzia saa sita mchana mpaka saa tatu usiku na baadaye tukasafirishwa kwa gari la polisi kwenda Lindi mjini ambako tulifika kwenye saa saba usiku na kukaa ndani hadi asubuhi.

Viongozi wa chama kutoka makao makuu walihakikisha kwamba mwanasheria wa chama anafika, alisafiri usiku kucha ili kututetea na mwanasheria huyo alipofika, juhudi za dhamana zikaanza na ilipofika saa 10 jioni, tukawa tumepewa dhamana.

Sasa, kama nilivyoeleza katika mkutano na wanahabari, kwanza; Jeshi la Polisi lilifanya makosa makubwa kutukamata na kuvunja mkutano wetu kwa sababu tulikuwa na mkutano halali, ulikuwa ni mkutano wa ndani kupokea wanachama na kueneza sera za chama, jambo ambalo linaruhusiwa kwa mujibu wa sheria.

Wala hatukuandamana kama ambavyo polisi wanadai. Kwa hiyo, kitendo cha polisi kuuvamia mkutano wetu, kutukamata, usumbufu, vyote havivumiliki.

Haya yanafanyika dhidi ya upinzani lakini wengine wanaendelea na shughuli zao kama kawaida, vile vyama tu ambavyo vinasimama na wananchi ndiyo vinaonekana shughuli zao kuzuiwa. Kwa hiyo, hili ni tukio ambalo tunalilaani kwa nguvu zetu zote na tunawataka Jeshi la Polisi waache kuingia kwenye mchakato wa siasa.

***SWALI: Kipi unajivunia katika maisha yako ya ubunge?***

**ZITTO:** Kuna vitu vingi sana ambavyo nimefanya nikiwa Mbunge wa Kigoma Mjini na kabla ya hapo Mbunge wa Kigoma Kaskazini. Na ni ukweli kwamba siyo peke yangu, bali kwa kushirikana na viongozi wengine na vilevile kutokana na misaada ambayo tunaipata kutoka sehemu mbalimbali za dunia kwa ajili ya kubadilisha hali ya maisha ya watu wa Kigoma.

Sasa, hivyo vitu ni vingi sana, nikianza kuvitaja hapa, sitamaliza kwa sababu kuna vitu ambavyo vinahusiana na maisha ya watu moja kwa moja kwa maana ya masuala ya elimu, afya... lakini vilevile kuna vitu ambavyo vinahusiana na maendeleo ya kimiundombinu na uwekezaji katika Mji wa Kigoma.

Mimi kwangu jambo kubwa ambalo ninajivunia kuliko yote katika kazi zangu za kisiasa kuwawakilisha watu wa Kigoma, ni heshima ambayo watu wa Kigoma wanayo nchini kwa kuwa na kiongozi ambaye ana msimamo kutetea kila sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na hili kwangu ndiyo la muhimu sana.

Zamani ilikuwa watu wa Kigoma wakienda nje ya Mkoa wa Kigoma, wanaona aibu kujisema kwamba wanatoka Mkoa wa Kigoma. Sasa hivi watu wa Kigoma wanaona ufahari kusema kuwa wanatoka Kigoma na hii ni sehemu ya kazi kubwa sana ambayo tumefanya kuonyesha kuwa Kigoma ni sehemu ya Tanzania na watu wa Kigoma wanastahili haki kama watu wengine wote, lakini bado hatujafikia mwisho kwa sababu bado kuna manyanyaso, ukandamizaji na kunyanyapaa, yote haya tutaweza kuyakamilisha kwa kuendelea kufanya kazi.

## HABARI KITAIFA



Mratibu wa mwitikio wa viongozi wa dini kutoka Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), Jovin Riziki, akizungumza na Baraza la Viongozi wa BAKWATA (hawapo pichani), Mkoa wa Morogoro, wakati wa uchaguzi wa viongozi wapya uliofanyika Masjid Ijumaa, Manispaa ya Morogoro. Ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa Hebu Tuyajenge, unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ufaransa yaipa Tanzania bil. 600/- za miradi mitatu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) zimesaini mikataba ya mkopo ya kutekeleza miradi mitatu ya kipaumbele ya umeme na maji inayokadiriwa kufikia Sh. bilioni 600.

Mikataba hiyo ilisainiwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, kwa niaba ya serikali na Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier na Mkurugenzi Mkazi wa AFD, Stéphanie Mouen.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, James aliainisha miradi hiyo ni wa usambazaji umeme vijijini ambao utagharimu Euro milioni 100 (sawa na Sh. bilioni 257.64) na utasambazwa katika mikoa 16 ya Tanzania Bara.

Alisema una lengo la kuhamasisha ukuaji mpana wa uchumi, kuongeza vipato vya watu wa vijijini na kuongeza ubora wa maisha na ustawi wa jamii vijijini.

"Utajikita katika kuunganisha umeme majumbani, taasisi, vituo vya usambazaji wa maji na biashara, ambapo matarajio ni kufikia makazi 3,788 katika vijiji 1,304 kwenye mikoa 16 ya Tanzania Bara.

"Utahusisha kujenga njia za umeme zinazofikia kilometa 3,949.5, kuweka transfoma 1,291 zenye ukubwa wa kVA 50, transfoma 876 za kVA 10, transfoma 464 za kVA 200 na kuunganisha wateja 81,957."

James alitaja mradi wa pili kuwa ni wa umeme wa kuunganisha Tanzania na Zambia ambao utagharimu Euro milioni 100 (sawa na Sh. bilioni 257.64).

Alisema mradi huo ni kwa ajili ya kuchangia uunganishaji wa mashirika ya umeme ya kusini mwa Afrika na mashirika ya umeme ya Afrika Mashariki.

Alisema unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400 na vituo vya kupoozea umeme katika ushoroba wa Iringa-Kisada -Mbeya -Tunduma - Sumbawanga.

Alitaja mradi wa tatu ni wa kazi za nyongeza kwenye mradi wa majisafi na majitaka katika miji inayozunguka Ziwa Victoria ambazo zitagharimu Euro milioni 30 (sawa na Sh. bilioni 77.29) na itahusisha maeneo ya Buhongwa, Kisesa, Buswelu katika jijini la Mwanza.

Alisema kiwango cha uzalishaji wa maji katika Jiji la Mwanza kupitia chanzo cha Kusini mwa jiji hilo ambacho ni mtambo wa kuzalisha maji wa Butimba kinatarajiwa kuwa mita za ujazo 20,000 kwa siku.

"Kupitia mkopo huu wa nyongeza mtambo huu wa kuzalisha maji utaongezewa uwezo wa kuzalisha kati ya mita za ujazo 40,000 hadi 45,000 kwa siku, na kuwezesha kupatikana kwa maji ya kutosha kwa maeneo yaliyotajwa ambayo hayakuwapo kwenye mradi hapo awali," alisema.

James alibainisha kuwa miradi hiyo yote iliyosainiwa inawiana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025, ambayo inaongoza juhudi za kuleta maendeleo nchini.

Alisema kwa sasa inatekelezwa kupitia Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP II) 2016/17 - 2020/21.

"Napenda kumshukuru Rais John Magufuli kwa kuendelea kudumisha uhusiano mzuri kati ya Tanzania na Ufaransa, uhusiano huu umefanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali zikiwamo sekta za maji na nishati," alisema.

Mkurugenzi wa AFD, Mouen alisema Ufaransa imedhamiria kuisaidia Tanzania katika jitihada za kufikia uchumi wa kati wa maendeleo.

Alisema mwaka 2019 ulikuwa wa historia ambapo Euro milioni 170 zilipitishwa na shirika hilo kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania na Euro milioni 300 nazo zimeshasainiwa.

Alisema wanaamini mwaka 2021 utakuwa ni wa utekelezaji wa miradi yote muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Naye Balozi Clavier alisema kwa miaka hiyo miwili wameona Ufaransa na Tanzania zikisaini makubaliano ya mikopo mikubwa ya kusaidia miradi ya maendeleo.

# Kada CCM ataka wagombea binafsi

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imeshauriwa kuangalia uwezekano wa kuruhusu kuwapo mgombea binafsi, ili watu ambao hawako kwenye vyama vya siasa waweze kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Ushauri huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alipokuwa akizungumzia hali ya kisiasa nchini.

Alisema, baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa huwa hawapendi kuona watu wanaokubalika kwenye jamii wakipewa nafasi ya kuongoza na huwawekea mizengwe na kuwakwamisha.

"Ninadhani umefika wakati sasa serikali kuangalia upya uwezekano wa kuwa mgombea urais, ninaamini kwamba wapo watu wengi tu ambao wanaweza kuwania uongozi bila kupitia vyama," alisema Ngawaiya.

Ngawaiya ambaye ni kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema kuna watu wanaamini wana uwezo wa kuongoza, na kwamba wasiachwe nyuma bali wapewe nafasi kwa kuruhusu mgombea binafsi ili watoe mchango wao kwa taifa.

"Sitaki kutaja chama, lakini vipo vyama ambavyo unaweza kukuta kiongozi wake anajua kuwa mwanachama fulani wananchi wanamtaka na anaweza kumfunika, hivyo anafanya kila njia kumzuia," alisema Ngawaiya, ambaye amewahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Kilimanjaro.

Ngawaiya alisema, njia pekee ya kumaliza sintofahamu hiyo ni kuruhusu kuwapo kwa mgombea binafsi, ili kumaliza mkanganyiko huo wa muda mrefu ambao naona kuwa haupaswi kuendelea kuwapo nchini.

Alisema, tangu akiwa Mbunge wa Moshi Vijijini alitoa wazo la mgombea binafsi wakati huo Msajili wa Vyama vya Siasa akiwa ni Jaji John Tendwa, na kwamba bado anaamini kuwa wazo hilo lina umuhimu.

"Tendwa alielekea kuona wazo langu kuwa ni jambo jema, lakini muda wake wa uongozi uliisha na mimi ubunge wangu ukaisha, hivyo wazo hilo likawa limeishia hapo bila msukumo," alisema.

Kada huyo alisema, ameamua kukumbushia tena wazo lake hilo la tangu mwanzoni mwa mwaka 2000, huku akihoji kwamba kuna kosa gani kuwa na mgombea binafsi?"

Alisema, kuna haja ya kupeleka muswada bungeni, ili kuruhusu mgombea binafsi ili alete changamoto, na kwamba kama yupo wa kushinda atashinda tu, hivyo hakuna haja ya kuendelea kuzuia hilo.


**KUPOTEA KWA KADI**

**Albert Elishamia Kimaro** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK X** yenye namba ya usajili **T992 AXS** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **TAN/RB/480730/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 25/2020**

**Ombi la FATMA ABDULKADIRI kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu ASHA HAJI AHMED**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 13/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 18/6/2020.

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

115792602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 59/2020**

**Ombi la IBRAHIM GEORGE kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu ZUWENA ABRAHAMAN AHMED**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 23/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 26/6/2020.

Sahihi ya Hakimu

115792502

**KUPOTEA KWA KADI**

**Mariam Athuman Makange** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji aina ya **TVS** yenye namba ya usajili **MC 940 BVK** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/CHA/RB/459170/2020**

115792902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhusiano mwema uwe msingi kuinua taaluma Gairo

WIKI iliyopita gazeti hili liliripoti kwa kina habari ya walimu wa Shule ya Sekondari Iyongwe, Kijiji cha Chihwaga Kata ya Itaragwe, wilayani Gairo, mkoani Morogoro, kupigwa mishale na watu wasiojulikana na mmoja kupoteza maisha.

Aidha, mwalimu mmoja akiwa hospitali kuuguza majeraha baada ya kushambuliwa akitoka kwenye shughuli zake eneo lile lile aliloshambuliwa mwalimu mwenzake.

Tukio hilo linadaiwa ni la kulipiza kisasi kwa kuwa mwalimu wa pili alikubali kutoa ushahidi polisi dhidi ya mwenziye aliyeuawa, jambo linalodaiwa kuwaudhi waliotenda kosa hilo.

Mwalimu huyo alieleza lengo la wahusika lilikuwa kumuua, lakini alichomwa mkuki kwenye mkono.

Mwalimu wa kwanza aliuawa Februari 24, mwaka huu na mwingine alijeruhiwa Juni 20, wote kutoka shule moja jambo ambalo lililozua taharuki na hofu kwa walimu waliobaki.

Baada ya vyombo vya habari vya IPP kuripoti kwa kina tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani humo, alifanya ziara na kuzungumza na wananchi wa eneo hilo, ikiwamo kusalimisha silaha za jadi ambazo zinatumika kushambulia walimu hao.

Tunapongeza uamuzi wa Jeshi la Polisi kuweka kikosi maalum kinachoongozwa na Mkuu wa Upelelezi Mkoa, na sasa hatua za kisheria zitakuchukuliwa kwa wote waliohusika.

Tunaamini pamoja na hatua hizi za ngazi ya mkoa katika eneo hilo kuna viongozi wa wilaya ambao ni Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na viongozi wengine wa vyombo vya ulinzi na usalama ambao wanaunda kamati ya ulinzi na usalama.

Pamoja na hatua zilizochukuliwa na jeshi hilo kufanya uchunguzi, bado kuna uhasama baina ya walimu na wenyeji huku wote wakitegemeana. Walimu wanatakiwa kufanya kazi wapate mshahara na wazazi wanahitaji watoto wao kufundishwa.

Kama walimu watashindwa kuishi kwa amani, hawataweza kufanyakazi inavyotakiwa, watashindwa kuwafundisha kwa moyo wanafunzi ambao wanatokana na jamii hiyo.

Hali hiyo ya uhasama ikiachwa kuendelea bila kutibu majeraha yanayoonekana na yasiyoonekana katika kujenga uhusiano mwema, kuna uwezekano mkubwa wa shule hiyo kuporomoka kitaaluma.

Matukio ya kushambulia watumishi wa umma au binadamu mwingine ni lazima yakemewe, zipo njia za kisheria za kufuata kupata suluhu ya tatizo lililopo kuliko kutoa uhai wa mtu au kujeruhi yeyote.

Ni vyema hatua zikachukuliwa kuhakikisha uhusiano mwema unarejea katika kijiji hicho, kwa kufanya vikao vya mara kwa mara na mambo yanayoweza kuwaunganisha.

Bila kufanya hivyo bado kutaendelea kuwa na visasi kwa walimu na jamii hiyo, matokeo yake ushirikiano wa kuboresha kiwango cha taaluma utakuwa mgumu.

Kwa mujibu wa taratibu shule, kamati au bodi ambayo huundwa na wazazi, walimu na viongozi wa eneo hilo ni kusimamia maendeleo ya shule na kujenga ujirani mwema, hali inapokuwa tofauti ni lazima uhusiano wa pande hizo utayumba.


Uhusiano mwema ndiyo nguzo ya kuifanya shule hiyo kufanya vizuri kitaaluma, ni wajibu wa jamii husika kurejesha hali ya amani na kuwa wa kwanza kufichua waliohusiana na mauaji hayo.

Vyombo vya habari vimetimiza wajibu wake wa kuisaidia jamii na matokeo yameonekana, kwa viongozi kuingilia kati ni ushahidi tosha kuwa kazi iliyofanywa inakwenda kutatua changamoto ya eneo hilo.

Huu utakuwa mwanzo wa kujenga uhusiano mwema baina ya pande zote na kuifanya shule hiyo kuandika historia na kuwa ya mfano wa ushirikiano wa kukuza taaluma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Zinahitajika hamasa kujenga miundombinu wenye ulemavu



Na Sabato Kasika

KATIKA kuhakikisha wanafunzi wa kike wa shule za msingi na sekondari wanasoma bila kupata changamoto ya kukosa masomo wakati wa hedhi jitihada mbalimbali zimefanyika zikiwamo kutoa hoja binafsi bungeni kuomba punguzo la gharama ya taulo za kike.

Miongoni mwa jitihada hizo au kampeni za kuchangisha fedha kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kununua taulo hizo ambazo zinatajwa kuwa suluhisho la tatizo hilo kwa wanafunzi wa kike zimefanyika hivi karibuni na huenda zitaendelezwa.

Kampeni ya kuchangia taulo hizo iliwahi kufikishwa bungeni na Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, Upendo Peneza na kuungwa mkono na wabunge wengine.

Lakini pamoja na hayo, ipo haja sasa kampeni kama hizo kuhamia kwenye miundombinu ya walemavu katika shule ili nao waweze kusoma bila changamoto ambazo ziko ndani ya uwezo wa jamii.

Ninasema hivyo kwa sababu elimu inatakiwa kutolewa kwa kila mtoto bila kujali tofauti za jinsia na kimaumbile, hivyo kuna haja ni muhimu kuondoa vikwazo vya baadhi ya shule kutokuwa na miundombinu ya kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kupata elimu bila tatizo lolote.

Wanafunzi wenye walemavu wa viungo hukutana na changamoto hasa wakati wa kwenda chooni, kutokana na kujengwa bila kuzingatia mahitaji yao na kusababisha watembee juu ya vinyesi na maji machafu ya chooni. Lakini wanahitaji viti mwendo ili kutembea hasa kwa wale ambao muda wote wanalala au kukaa chini kutokana na matatizo ya miguu na uti wa mgongo.

Tatizo lipo pia kwenye baadhi ya madarasa ambayo nayo ni vyema yajengwe kulingana na mahitaji ya walemavu hasa wa viungo vya miguu, kwani wapo wanaotembea kwa kusota chini.

Kwa ujumla ulemavu si dhambi wala laana bali ni hali inayompata yeyote na inayotakiwa anayepata shida hiyo kuwezeshwa kwa kuangalia mahitaji ya msingi ikiwamo elimu na miundombinu rafiki ya kupata elimu.

Hivyo, katika kujenga jamii yenye usawa na kujali makundi yote, ni vyema kutambua kuwa si jukumu la serikali tu kuboresha miundombinu ya shule kwa ajili ya wanafunzi walemavu bali nayo inahusika.

Karibu shule zote zina uhaba wa madarasa na vyoo, hivyo vinapofanyika juhudi za ujenzi ambao kimsingi unahusisha jamii, ni muhimu kuzingatia miundombinu ya wanafunzi wa aina hiyo.

Inawezekana katika mazingira hayo ya kutokuwapo kwa miundombinu ya walemavu shuleni, wapo baadhi ya wanafunzi ambao wameacha shule na kushindwa kufikia malengo yao ya baadaye waliojiwekea.

Jamii ihamasishwe kushiriki ujenzi wa madarasa na vyoo, lakini kikubwa ikiwa ni kuzingatia kuwapo kwa miundombinu inayogusa walemavu wa viungo ili nao wajione kama wanathaminiwa. Kampeni zisiishie katika kuchangia taulo za kike tu, bali zihamie pia kwenye ujenzi wa miundombinu ya shule kwa ajili ya wanafunzi walemavu wakiwamo wa kike na wa kiume.

Ukweli ni kwamba ukosefu wa miundombinu ya shule kwa makundi yote ni kikwazo kwa wanafunzi wenye ulemavu kupata elimu, hivyo wadau wote wa elimu hawana budi kuliona tatizo hilo na kushiriki kikamilifu kulimaliza.

Kuwapo kwa miundombinu ya walemavu katika shule kuna mchango mkubwa hasa kufanikisha jitihada za serikali za kuwa na elimu jumuishi ambayo inahusisha wanafunzi wote wakiwamo wazima na wenye ulemavu.

Hivyo ni wakati sasa shule zote, kwa dhana ya elimu jumuishi iwekwe miundombinu ya kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kujumuika na wenzao wazima ili kuzoeana na kuweka usawa. Ninaamini kwamba hilo litawezekana, hasa zikifanyika kampeni maalum za kuhamasisha jamii kushiriki kwa hali na mali katika ujenzi wa madarasa na vyoo vinavyozingatia mahitaji ya kundi hilo.

Ikiwa kila mmoja atashiriki katika jambo hili, atarahisisha safari ndefu ya kuelekea katika lengo la kuwa na elimu inayofikiwa na watoto wote bila kujali ni wazima au ni walemavu wa viungo ili wote wafaidike na elimu.

Ikumbukwe hata Mpango wa Umoja wa Mataifa (UN) unaozitaka nchi wanachama kuhakikisha elimu inatolewa kwa kila mtoto bila kujali tofauti za jinsia na kimaumbile.

Vilevile mkakati huo uliosimamiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na kuishia mwaka 2015, ulilenga kuimarisha mpango wa elimu kwa wote katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kwa watoto wote, vijana na watu wazima, hivyo kuna haja ya kutafakari tulikofikia na kuchukua hatua.

# Wafanyabiashara wadaiwa kuficha petroli

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

BAADHI ya wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, wamelalamikia wafanyabiashara wa mafuta ya petroli kuyaficha na kusababisha kupanda kwa gharama za usafiri wa vyombo vya moto, hali inayodaiwa kujitokeza kutokana na uhaba wa mafuta.

Mmoja wa wananchi hao Flora Mwaga, mkazi wa kitongoji cha Majengo, alisema usafiri wa mizunguko ya ndani ya mji huo imepanda ghafla kwa nauli ya bodaboda na Bajaji, maradufu.

"Tulikuwa tukipanda bajaji kutoka mjini hadi huku Majengo kwa Sh. 500 sasa tunalipa 1,000 kuna maeneo mengine tunalipa hadi Sh. 2,000 badala ya 1,000 kitu ambacho kinatuumiza sana sisi wananchi wenye kipato kidogo...tunaziomba mamlaka zinazohusika kuingilia kati na kutatua changamoto hii," alisema Flora.

Mmoja wa waendesha pikipiki, George Peter, alisema wanalazimika kupandisha bei ya usafiri kutokana na kukosekana kwa mafuta katika vituo vinavyotoa huduma hiyo na kudai baadhi ya wafanyabiashara waliolangua mafuta hayo na kuyaweka ndani wanauza kwa kificho kwa bei ya Sh. 2,500 kwa lita.

"Sisi hatuna namna inabidi tupandishe bei tu ya nauli ili kufidia gharama ya ununuzi wa mafuta...kitu cha msingi serikali itusaidie kutatua changamoto ya mafuta kwa kuwa inavyooneka mafuta yapo, lakini wamiliki wa vituo vya mafuta wameyaficha ndani ili bei ikipanda wayauze," alisema Peter.

Kwa upande wake, Mkaguzi wa petroli kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jakson Makaya, alikiri kuwapo kwa changamoto ya uhaba wa mafuta kutokana na wafanyabiashara na waagizaji kupunguza kasi ya uagizaji wa bidhaa hiyo.

Alisema hiyo inatokana na biashara kusuasua katika kipindi cha mlipuko wa virusi vya corona, hivyo kudai kwamba tayari mafuta yameagizwa kwa kiasi kikubwa na huenda changamoto hiyo ikaisha katika kipindi kifupi kuanzia sasa.



Taka zinazozalishwa na wafanyabiashara wadogo zikiwa zimetupwa katika mtaro wa maji ya mvua katika Barabara ya Kilwa, eneo la Mtoni Mtongani, jijini Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho kinachangia uchafuzi wa mazingira. **PICHA: SABATO KATIKA**

# Bodaboda mafataki wapewa angalizo

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amewaonya waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda kuacha mara moja uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi hasa wa shule za msingi na sekondari.

Wameonywa kuwa vitendo hivyo vitawaharibia maisha, kujikuta wakiishia jela na kuziacha familia zao zikiteseka bila msaada.

Wangabo, alitoa onyo hilo wakati akikabidhi mkopo wa pikipiki 35 kwa waendesha bodaboda ambao ni wanachama wa New Bodaboda Saccos iliyopo Manispaa ya Sumbawanga.

Pikipiki hizo zilitolewa na Manispaa hiyo ukiwa ni utekelezaji wa kutoa mikopo isiyo na riba kwa makundi maalum ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika Manispaa hiyo.

Alisema baadhi ya waendesha bodaboda hao wamekuwa na tabia ya kuwa na uhusiano ya kimapenzi na wanafunzi, kitendo ambacho ni hatari kwao, na kuwa yeye kama mkuu wa mkoa huo, hatakubali kuona vitendo hivyo ambavyo vinaharibia masomo wanafunzi vikiendelea.

"Wapo baadhi yenu mekuwa kikwazo katika kampeni yetu inayoitwa 'Mwache mtoto asome' kwani mmekuwa mkijihusisha na wanafunzi kimapenzi, siwezi kuwavumilia......huwa ninawaona mnawabeba wanawake wakubwa, tena warembo kweli wamevaa na mawigi wamependeza si hao wawe wapenzi wenu, muwaache wanafunzi wasome," alisema.

# Magugu maji ya Ziwa Victoria yaiibua NEMC

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

MWENYEKITI wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Prof. Esnati Chaggu, amesema jitihada za udhibiti wa gugu maji katika Ziwa Victoria zishirikishe wadau wote wa mazingira ili ziwe endelevu na kuleta matokeo chanya.

Akihitimisha ziara ya Bodi na Menejimenti ya Baraza hilo Kanda ya Ziwa kwa lengo la kukagua athari za kimazingira katika Ziwa Victoria kutokana na ziwa kujaa kwa kina cha maji na kuongezeka kwa magugumaji ambayo yanaathari kubwa kimazingira, Prof Chaggu alisema juhudi za

makusudi zinahitajika kutoka kwa wadau.

"Taasisi ziendelee kushirikiana ili kuleta tija ya kazi hii, aidha turejee kwenye sera zinazohusu udhibiti wa viumbe vamizi kama gugu maji kwa ajili ya kukabiliana nao ili kulinda ziwa lisiharibiwe na gugumaji," alisema Prof. Chaggu

Amepongezea Wakala wa Elimu na Mafuzo ya Uvuvi Tanzania (FETA) tawi la Nyegezi kwa kuendeleza mafunzo kwa vijana juu ya kukabiliana na gugumaji kwa kutumia mdudu aitwae Mbwawa kavu ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa LVEMP I na II.

"Muhimu tuendeleze mradi huu wa kuzalisha mbawa kavu ambaye ni mrafiki kwa mazingira atakayesaidia kuondoa gugumaji katika Ziwa Victoria," alisema Prof. Chaggu na kuongezea kuwa mradi utazamwe kwa jicho la tofauti ili uendelezwe.

Amesema Ziwa Victoria lina umuhimu mkubwa kiuchumi kwa ngazi ya wananchi na Serikali kwa ujumla hususani shughuli za uvuvi na usafirishaji, gugumaji litakapo achiwa litasababisha shughuli hizi kukwama na kupelekea hasara, hivyo ni jukumu la kila mdau wa maendeleo kuhakikisha anashiriki katika kuendeleza juhudi za FETA katika kutokomeza gugumaji vamizi.

Mjumbe wa Bodi ya NEMC, kutoka TPRI, Dk. Neduvoto

Mollel, alifafanua umuhimu wa kuzalisha mdudu aitwae Mbawa Kavu kwa wingi ambaye atatumika kuyaangamiza magugu maji hayo kwani mdudu huyo ni rafiki kwa mazingira.

Kaimu Mkurugenzi wa FETA-Nyegezi mkoani Mwanza, Mukama Ndaro, alisema changamoto kubwa ni rasilimali fedha za kuwezesha vijana waliopata mafunzo kuendeleza zoezi la kudhibiti magugu ndani ya ziwa.


BISMILAH RAHMAN RAHIM



615793102

Familia ya Marehemu **Dk. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea Marehemu Dk. Omar Ali Juma itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **2 Julai, 2020** saa kumi jioni katika Msikiti wa Ngazija.

Ndugu, marafiki na Jamaa wote Mnakaribishwa Kufika kwenu ndio mafanikio yetu.

Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

**AMIN**



# Wanafunzi walioathiriwa na corona kusaidiwa kisaikolojia

**Na Elizabeth Zaya**

WALIMU wa shule kadhaa za msingi katika Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, wamepatiwa mafunzo ya namna ya kutoa huduma ya kisaikolojia kwa wanafunzi wa shule hizo walioathiriwa na uwapo wa ugonjwa huo kwa miezi mitatu waliyokaa nyumbani.

Mafunzo hayo yalitolewa mwishoni mwa wiki na Shirika linaloshughulika na masuala ya watoto la Save the Children Tanzania yakilenga kuwajengea walimu hao uwezo wa kuja na mbinu mbadala za kufundisha ambazo zitasaidia kuwaondoa wanafunzi katika fikra za ugonjwa huo katika kipindi chote watakachokuwapo shuleni.

Meneja Programu wa Save the Children Tanzania, Jesca Ndana, alisema wanaamini mafunzo hayo ni muhimu kwa walimu katika kipindi hiki ambacho shule zimefunguliwa baada ya kufungwa kwa kipindi kirefu kutokana na corona.

"Tunaamini mafunzo haya pia yatasaidia walimu namna ya kuwa karibu na wanafunzi na kuwasaidia kisaikolojia. Kuna baadhi ya wanafunzi ambao walikumbana na changamoto zilizosababishwa na ugonjwa wa corona ikiwamo kubakwa, kupigwa na nyingine nyingi," alisema Ndana.

"Kitu cha msingi ambacho tunataka walimu wazingatie sana ili kuwasaidia wanafunzi waliokumbana na changamoto hizo ni kuwapatia huduma ya kisaikolojia na tunaamini kwamba itawarudisha katika hali yao ya kawaida."

"Tunafahamu kwamba ugonjwa wa corona umeacha hofu kubwa kwa watoto na kuna uwezekano kwamba hata baada ya kuisha wapo baadhi ambao huenda wakawa wanaogopa na kutamani kuendelea kubaki nyumbani, kwa hiyo tunaamini kwamba kupitia mafunzo haya, walimu watawasaidia watoto wasiendelee kuwa na hofu ya ugonjwa,"alisema Ndana.

Azekiel Nichombe, mmoja wa walimu waliopatiwa mafunzo hayo akitokea Shule ya Msingi Changanyikeni, jijini Dar es Salaam, alisema mbinu walizopewa na shirika hilo ni muhimu na zitawasaidia watoto shuleni.

Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi ya Makongo, Magdalena Machunga, alisema wamejiandaa kuhakikisha watoto wanakuwa salama wakati wote watakaokuwa shuleni.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Francisca Makoye, aliwasisitiza walimu hao kuwa rafiki na karibu na wanafunzi hao ili pale wanapokutwa na changamoto yoyote wasiogope kuwaeleza.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja linalounganisha maeneo ya Kata ya Keko Magurumbasi na Keko Mwanga, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ili kuwaondolea wananchi changamoto ya kukosekana kwa mawasiliano ya barabara wakati wa mvua. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Pilipili kichaa kuwakomboa wana-Ikungi

**Na Jumbe Ismailly, IKUNGI**

WANANCHI wa kitongoji cha Kipunda, kijiji cha Mtunduru wilayani hapa, wamepata mkombozi wa kilimo cha pilipili kichaa baada ya kuzinduliwa soko la zao hilo.

Soko hilo limezinduliwa na Kampuni ya Vegrab Organic Farming Ltd., kwa kushirikiana na kampuni inayouza matrekta Agricom.

Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Gladness Nyange, alisema soko la zao la pilipili kichaa ni kubwa kinachotakiwa ni uzalishaji mkubwa na wenye ubora zaidi.

"Mimi nina imani na zao hili litatupeleka mbali sana kupitia juhudi ile tulioanza nayo, tuendelee nayo, kwani masoko ni makubwa, lakini yanataka uzalishaji pia wenye ubora," alisisitiza.

Nyange alisema Mkoa wa Singida unaweza kuwa kituo kikubwa cha uzalishaji wa pilipili kichaa ndani ya Afrika Mashariki kama jitihada zitawekwa na kuongoza Afrika kwa uzalishaji wa zao hilo.

Alifafanua kuwa mazingira pamoja na ardhi iliyopo katika Mkoa wa Singida inadhihirisha kwamba pilipili itakayozalishwa kwenye maeneo yote ya Mkoa wa Singida itakuwa nzuri kuliko inayotoka sehemu yoyote Tanzania na Afrika Mashariki.

Akizindua mnada wa soko la pilipili kichaa, Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Gurisha Msemo, alisema kampuni inayonunua zao hilo imesaini mkataba wa miaka mitatu na kwa msimu wa 2019/2020, kampuni hiyo itanunua pilipili kichaa iliyoiva kwa bei ya Sh. 4,500 kwa kilo moja na Sh. 5,000 kilo moja kwa pilipili mbichi.

Msemo alitoa sababu za soko la zao hilo kuzinduliwa katika Kata ya Mtunduru kuwa ni kutokana na idadi kubwa ya wakulima wa zao hilo na kati ya wakulima 159 waliolima pilipili kichaa, 110 ni wakulima kutoka Wilaya ya Ikungi.

Mwenyekiti wa Kipunda AMCOS, Omari Nyuda, kwa kutumia kaulimbiu ya 'Ongeza tija pilipili inalipa' alisisitiza uzalishaji bora wa zao hilo ili waweze kuendelea kupata fedha nyingi zaidi.

# Taasisi DIT yataka vijana kuchangamkia fursa gesi

**Na Agnes Temu**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imewataka vijana waliopata stashahada na shahada ya uhandisi kusomea kozi fupi ya mfumo wa kuweka gesi kwenye magari ili kujiajiri na kuajiri wengine.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Gesi Asilia wa DIT, Dk. Esebi Nyari, wakati akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam.

Alisema vijana hao zaidi ya 300 watajifunza kufunga gesi kwenye magari na kukagua mfumo wa ukarabati huo, ili kurahisisha kasi ya kuhudumia wateja wanaoongezeka kila siku.

"Unajua mfumo huu ni mpya hapa nchini umeanza tangu mwaka 2018, ila wateja wameongezeka mwaka huu magari 350 tayari yana mfumo, hatutoi injini wala hatutoi mfumo wa kawaida wa kuweka mafuta tunaongeza kifaa kipya ili mtumiaji achague atumie gesi au petroli," alifafanua Nyari.

Alisema kumekuwa na upungufu wa wataalamu wa kufunga mfumo wa gesi asilia kwenye magari, kutokana na kitengo hicho kuwa na mtaalamu mmoja ambaye ndiye aliyefanya utafiti na kugundua mfumo huo.

Alisema mfumo huo unatumika kwenye magari ya petroli na gharama za kuweka mfumo wa gesi kwa magari madogo yenye 'cylinder' nne ni Sh. 1,800,000 na 'cylinder' sita ni Sh. 2,200,000 na wateja wengi wanaotumia mfumo huo ni magari mtandaoni.

Alisema dereva anayetumia petroli anasafiri kilomita 12 kwa saa wakati akitumia gesi anatembea kilomita 20 kwa saa na kwamba kutumia gesi kunazuia uchafuzi wa mazingira.

**HABARI KITAIFA**

# Wanafunzi waishauri TAKUKURU taarifa za rushwa ngono vyuoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wanaosoma vyuo mbalimbali mjini Shinyanga, wameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, kuwahakikishia usalama wa maisha yao, kwa kutunza siri za taarifa za rushwa ya ngono pale wanapokuwa wakizitoa kwenye taasisi hiyo.

Hayo yalibainishwa juzi na wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali mjini Shinyanga, wakati wa utoaji elimu ya kutokomeza rushwa ya ngono vyuoni iliyokuwa ikitolewa na TAKUKURU.

Wanafunzi walioshiriki mafunzo hayo ni kutoka Chuo cha Ualimu Shycom, Chuo cha Ufundi Stadi Veta, pamoja na Chuo cha Ushirika Moshi tawi la Kizumbi mkoani Shinyanga.

Baadhi ya wanafunzi hao akiwamo, Betina Mwashambwa kutoka Chuo cha Ushirika Moshi tawi la Kizumbi mkoani Shinyanga, alisema kuna wanafunzi wanaombwa rushwa ya ngono na wahadhiri wao, lakini wanaogopa kutoa taarifa hizo TAKUKURU, kwa kuhofia siri kuvuja na hatimaye kumharibia maisha yake.

"Tanaiomba TAKUKURU, mtuhakikishie usalama wa maisha yetu, kwa kutunza siri pale wanafunzi wanapokuwa wakitoa taarifa kwenu za rushwa ya ngono, kwa sababu unaweza kutoa taarifa kisha mhusika akaambiwa kuna mwanafunzi amekushtaki unamwomba rushwa, jambo ambalo litanifanya niishi maisha magumu chuoni," alisema Mwashambwa.

Mwenyekiti wa Klabu ya kupinga rushwa wa chuo hicho, Kombeho Wiliam, aliwataka wanachuo kuacha kutunza siri za kuombwa rushwa ya ngono, bali watoe taarifa hizo TAKUKURU ili wasaidiwe na kupata haki zao, na siyo kuendelea kunyanyaswa kingono na kupewa maksi za bure.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Shinyanga, Hussein Mussa, alisema wametoa elimu hiyo ya rushwa ya ngono kwa wanachuo, kwa sababu hatima ya ufaulu wao upo mikononi mwa wahadhiri, hivyo ni rahisi kwao kurubunika na kutoa rushwa hiyo.

Aidha, aliwatoa wasiwasi wanachuo hao kuwa taasisi hiyo itatunza siri kwa mwanafunzi yeyote ambaye atatoa taarifa za kuombwa rushwa ya ngono, huku akibainisha kuwa tangu wafungue dawati la rushwa ya ngono mwaka jana, wameshapokea taarifa mbili tu za wanachuo kuombwa rushwa hiyo.

**Wanafunzi walioshiriki mafunzo hayo ni kutoka Chuo cha Ualimu Shycom, Chuo cha Ufundi Stadi Veta, pamoja na Chuo cha Ushirika Moshi tawi la Kizumbi mkoani Shinyanga.**

# DC awaonya wanaoweka kadi za benki dhamana

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Selemani Mzee, amewaonya baadhi ya watumishi wa serikali wenye tabia ya kuchukua mikopo kwenye taasisi za fedha kwa kuweka dhamana kadi zao za benki (ATM) kuacha tabia hiyo.

Vilevile, amewaonya wakazi wa wilaya hiyo kuacha kuchukua mikopo kwenye taasisi hizo kwa kuweka dhamana mali ambazo siyo zao kama vile nyumba.

Aliyasema hayo wilayani Masasi alipokuwa akizungumza na wananchi wa wilaya hiyo wakati wa uzinduzi wa tawi la Taasisi ya fedha ya Yetu Microfinance wilayani Masasi.

**Baada ya wakopaji hao kuweka dhamana hiyo ya kadi za benki taasisi husika wanazokopa ndiyo hutumia kadi hizo kukata fedha za mikopo yao.**

Alisema wapo baadhi ya watumishi wa serikali ambao wamekuwa na tabia ya kukopa fedha kwenye taasisi za kifedha na dhamana zao wakiweka kadi za benki, sehemu ya makato ya mkopo wake taasisi husika ndio wanafanya kazi ya kwenda benki na kutoa fedha za mdaiwa.

Alisema baada ya wakopaji hao kuweka dhamana hiyo ya kadi za benki taasisi husika wanazokopa ndiyo hutumia kadi hizo kukata fedha za mikopo yao.

Alisema dhana ya kukopa kwenye taasisi za kifedha siyo mbaya kwani inalenga kujiinua kiuchumi, lakini jambo pekee ambalo wananchi ambao wanakwenda kukopa wanapaswa kusoma masharti ya taasisi husika kabla ya kukopa.

Mzee alisema kumekuwapo na migogoro mingi inayofika katika ofisi yake inayohusu suala la mikopo, ikiwamo mwananchi kukopa kwenye taasisi za fedha kisha kuweka dhamana mali ambazo siyo zake kama vile nyumba, gari.

Akisoma taarifa fupi ya benki hiyo, Meneja Mkuu wa Yetu Microfinace, Pendo Lauwo, alisema Yetu Microfinace inatoa huduma zote za kibenki.

Alisema katika kuhakikisha huduma zake bora zinapanuka zaidi wameona ni bora kuwasogezea huduma hizo kwa wakazi wa Wilaya ya Masasi na mikoa ya kusini kwa ujumla.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mabanda ya biashara ikiwa ni maandalizi ya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanahabari wapewa jukumu kuhamasisha chanjo ya watoto

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WANAHABARI nchini wametakiwa kutumia uweledi wa taaluma zao kuihamasisha jamii kutambua umuhimu wa kupeleka watoto katika vituo vya afya kupatiwa chanjo ya kujikinga na magonjwa kama vile surua, saratani ya mlango wa uzazi pamoja na polio.

Ofisa Mpango wa Taifa wa chanjo, Lotalis Gadau, aliyasema hayo wakati akitoa mafunzo ya siku moja kwa wanahabari kutoka mikoa ya Kagera na Geita.

Alisema Wizara ya Afya kupitia kitengo cha mpango wa Taifa wa chanjo, kimebaini kuwa kiwango cha mahudhurio ya chanjo kwa watoto wadogo walio chini ya umri wa miaka mitano na wasichana wa umri wa chini ya miaka 14 yamepungua tangu kuibuka kwa ugonjwa wa corona.

Alisema chanjo zilianzishwa mwaka 1975 kwa lengo la kutokomeza magonjwa kwa watoto ili kuwaepusha na madhara mbalimbali ikiwamo kifo.

Alisema chanjo kwa watoto ni muhimu kwani wasipopatiwa wanaweza kushambuliwa na magonjwa mbalimbali ikiwamo surua, rubella na hivyo kuwataka waanahabari nchini kwenda kuelimisha jamii sambamba na kuwahamasisha wazazi na walezi.

"Tumewaita wanahabari kuwapatia mafunzo haya kwa sababu tunatambua kuwa mna mchango mkubwa katika kuielimisha jamii, mpango wa Taifa wa chanjo tumebaini tangu ugonjwa wa corona uingie nchini, mahudhurio ya chanjo kwa watoto waliochini ya umri wa miaka mitano pamoja na wasichana wenye umri wa chini ya miaka 14 yamepungua kutokana na wazazi kuhofia kuaambukizwa corona," alisema Gadau.

Awali Mratibu wa Huduma ya Chanjo Mkoa wa Geita, Wille Luhangija, akitoa taarifa ya hali ya chanjo mkoani humo alisema tangu kuingia kwa ugonjwa wa corona hapa nchini mahudhurio ya chanjo yamepungua, wazazi wanahofia kuambukizwa ugonjwa wa corona.

Alisema mwaka 2019 Mkoa wa Geita ulifanikiwa kufikia asilimia mia kwa kutoa chanjo ya surua, rubella kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na asilimia 75 kwa wasichana wenye umri wa chini ya miaka 15.

# Waziri ataka uchunguzi mil. 400/- kituo cha afya

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameagiza kufanyika uchunguzi wa kina wa matumizi ya zaidi ya shilingi milioni 400 zilizotumika kujenga Kituo cha Afya Munzeze, wilayani Buhigwe mkoani Kigoma, baada ya kutoridhishwa na ubora wa majengo ya kituo hicho.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo alipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa kituo hicho ambacho kikikamilika kinatarajiwa kutoa huduma kwa zaidi ya wakazi 25,000 wa kata hiyo, wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo inayopatiwa fedha na serikali.

"Nakuagiza Mkuu wa Wilaya ya Buhingwe uanze kufuatilia matumizi ya fedha hizo na nitatuma timu ya uhakiki ili tuhakikishe kwamba shilingi milioni 400 zilizotolewa na serikali zilitumika vizuri au la," alieleza.

**Uhakiki huo ukibaini ubadhirifu, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa watu wote waliohusika na ubadhirifu huo na kuonya kuwa huu si wakati wa kubembelezana.**

Dk. Mpango alisema uhakiki huo ukibaini ubadhirifu, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa watu wote waliohusika na ubadhirifu huo na kuonya kuwa huu si wakati wa kubembelezana.

Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, Kanali Michael Ngayalina, alisema atayafanyia kazi maelekezo ya Waziri Mpango, kwa kuwa tayari alifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa ujenzi wa kituo hicho.

Aidha, alimshukuru Dk. Mpango kwa kufanya ziara katika wilaya hiyo katika jitihada za kuhakikisha fedha za serikali zinatumika kikamilifu katika miradi mbalimbali inayotekelezwa kwa manufaa ya wananchi.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya Munzeze ameiomba serikali itoe kiasi kingine cha shilingi milioni 123 kwa ajili ya kununua vifaa tiba ili kituo hicho kianze rasmi kutoa huduma kwa wananchi mapema mwezi Julai, 2020.

Conrad alisema ujenzi wa kituo hicho ulitakiwa kukamilika Machi, 2019, lakini ilishindikana kutokana na uwapo wa mvua nyingi zilizosababisha kushindwa kusafirisha vifaa kwenda eneo la ujenzi na changamoto ya ununuzi.

Kituo hicho cha Afya Munzeze kikikamilika kitaongeza idadi ya watu wanaohudumiwa katika zahanati iliyopo hivi sasa wapatao 16,000 hadi kufikia takribani wakazi 25,000 kutoka vijiji vinne vinavyounda kata hiyo vya Munzeze, Kishanga, Kigogwe na Murungu.

Katika hatua nyingine Dk. Mpango amewaahidi wananchi wa mkoa wa Kigoma kwamba serikali itajenga barabara inayoanzia katika mpaka wa Burundi na Tanzania kupita katika maeneo ya Wilaya ya Buhigwe, Kasulu, Kibondo na Kakonko, hivyo kuwawezesha wakazi hao kusafirisha bidhaa katika nchi jirani ikiwamo Uganda na Burundi.



Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi (katikati), akikata utepe kuzindua mkataba wa huduma kwa wateja toleo la nne la mwaka 2020, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Erick Shitindi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Adam Fimbo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Aenda jela miaka 7 kwa kumbaka mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa wa Wete imemhukumu kijana Juma Ali Hamad, mkaazi wa Maambani Kiuyu Wilaya ya Wete, kwenda kutumikia Chuo cha Mafunzo kwa muda wa miaka saba na kulipa fidia ya Sh. 300,000 baada ya kupatikana na hatia ya kutorosha na kubaka mtoto wa miaka 13.

Hukumu hiyo ilisomwa na Hakimu Abdallah Yahya Shamhuni, baada ya kuona kwamba ushahidi uliotolewa mahakamani haukuwa na chembe ya shaka.

"Mtuhumiwa umepatikana na hatia kwa makosa yote mawili, kosa la kwanza ambalo ni kutorosha utatumikia chuo cha mafunzo (jela) kwa miaka miwili na kosa la pili ni kubaka ambalo utatumikia miaka mitano pamoja na kulipa fidia ya shilingi 300,000," alifafanua hakimu Shamhuni.

Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP-Pemba), Mohamed Said Moahamed, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa, ili iwe fundisho kwake na kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Awali ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitenda makosa mawili ambapo kosa la kwanza alilitenda Mei 18, mwaka 2019 saa 2:20 asubuhi Maambani Kiuyu Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali na bila ya ridhaa ya wazazi wake, mshtakiwa huyo alimtorosha mtoto wa miaka 13 kutoka nyumbani kwao na kumpeleka kwenye nyumba anayoishi yeye.

Aidha, ilidaiwa kuwa siku hiyo hiyo saa 2:30 asubuhi Maambani Kiuyu, bila ya halali alimbaka mtoto huyo na kumsababishia maumivu.

## Wazazi Geita wataka vifaa kujikinga corona

**Na Sara Magesa,** GEITA

BAADHI ya wazazi wameiomba serikali kuweka vifaa vya kunawa mikono na sabuni shuleni pamoja na kifaa cha kupima joto kwenye lango la kuingia ili kuchukua tahadhari na kuzuia corona.

Ruben Makala na Stanford Juma, wakazi wa kijiji cha Nyakagwe wilayani Geita walisema pamoja na nia njema ya serikali ya kuwarudisha wanafunzi shuleni, ipo haja ya miongozo iliyotolewa na wizara kutobaki kwenye ofisi za elimu na badala yake ishuke hadi kwenye ngazi za jamii kuwaelimisha wanafunzi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki wakati wa kutoa elimu ya tahadhari ya namna ya kujikinga na corona iliyotolewa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Kuendeleza Wachimbaji Wadogo (FADev).

Aidha, waliiomba serikali kutengeneza mazingira yatakayowawezesha wanafunzi kunawa mikono kila mara wawapo shuleni hasa kwenye shule ambazo hazina huduma ya maji.

"Serikali imeamua kufungua shule, lakini wasiwasi wetu ni hawa wanafunzi watakuwa kwenye usalama kiasi gani, maana shule zetu hazina maji na sijui kama shule zimenunua ndoo za maji na hawa watoto wadogo nani atawasimamia kunawa serikali inapaswa kutoa mwongozo," alisema Rubein Saanane.

## 6,808 wafikiwa Dar kampeni TB

**Na Sabato Kasika**

JUMLA ya watu 6,808 kutoka kata tatu, jijini Dar es Salaam, wamefikiwa katika kampeni za siku 10 za nyumba kwa nyumba za kutoa elimu na kuhamasisha jamii na kupima ugonjwa wa kifua kikuu.


Kampeni hizo zilifanywa na klabu za TB, ambazo ziko chini ya Taasisi ya Mapambano ya Kifua Kikuu na Ukimwi Temeke (MUKIKUTE) yenye maskani yake Temeke.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki iliyopita, wakati wa kufunga siku 10 za kampeni hizo, Makamu Mwenyekiti wa MUKIKUTE, Seif Mchila, alisema, kampeni zilifanyika kata za Azimio, Kiburugwa na Keko.

"Kampeni hizo zilifadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Norway liitwalo LHL International, ambalo limesaidia kwa posho hadi tukafikia idadi ya watu hao ingawa kulikuwa na changamoto nyingi," alisema Mchila.

Alisema, walifikia idadi hiyo ya watu, lakini waliojitokeza kupima kifua kikuu wakawa wachache, hali ambayo inaonyesha bado kuna haja ya kuendelea kutoa elimu zaidi kuhusu dalili za ugonjwa huo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 30, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Ili kukabili msongamano masomo yawe kwa 'shifti'**



Ukurasa 14

**Pale serikali ilipoelekeza wadau nao wafunguka**



Ukurasa 13

Likizo ya corona ilivyoliza watoto

ELIMU

**NA BEATRICE PHILEMON**

# 'Serikali, jamii tusaidieni kubeba jukumu hili zito'

ILIKUWA saa 5:30 jioni Jumamosi wiki iliyopita nilipokwenda Chanika Lukooni wilayani Ilala, kumtembelea Upendo Michael, mama mwenye mtoto mlemavu kujadili changamoto zinazowakabili watoto wanaoishi na ulemavu na haki zao.

Nilipofika nilimkuta Upendo na mtoto wake mwenye ulemavu wa viungo wakiwa wananisubiri. Kijana huyo alikuwa amelala huku mama yake akiwasha mkaa kuandaa chakula cha jioni.

Mtoto wake Alex mwenye miaka 10 anaponiona anaanza kutabasamu, baadaye ninamshika mkono ili niongee naye lakini nilipojaribu kuzungumza naye mama yake ananiambia hawezi kuongea, kukaa wala kutembea, maisha yake yote ni kulala muda wote.

Akizungumza na Nipashe kwa uchungu, Upendo mama mzazi wa Alex Mponzi, anasema mwanzoni Alex hakuwa mlemavu. Alijifungua mwaka 2010 akiwa salama lakini alipofikisha miezi mitano ulemavu ulianza kujitokeza na mpaka sasa hakai wala kutembea.

Anasema mwaka 2016 aliwahi kumpeleka katika hospitali ya CCBRT kitengo cha mazoezi ili kufanya mazoezi ya viungo lakini kutokana na uwezo mdogo kifedha tena alikuwa akifanya kazi za ndani akilipwa mshahara kiduchu, alishindwa kuendelea kumpeleka kwenye mazoezi.

"Nilipenda sana mtoto wangu afanye mazoezi ya viungo lakini kipindi hicho mshahara wangu wa kazi za ndani ulikuwa mdogo, nauli ya kwenda na kurudi kila siku hospitali ilikuwa haitoshi na baba niliyezaa naye mtoto alinikimbia baada ya kuona amekuwa mlemavu," anasema kwa uchungu.



Alex katika umri wa miaka 10 yuko mikononi mwa mama yake Upendo. Familia hii inaomba jamii na serikali iwasaidie. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

**CHANGAMOTO ZA ALEX**

Upendo akirejea tena kwenye historia ya Alex anasema mtoto wake amekuwa na hali ngumu baada ya kushindwa kumsaidia na maisha yake hadi sasa yanaendelea kuwa magumu na mshahara wa utumishi wa ndani aliokuwa analipwa haukidhi mahitaji yake, hivyo aliamua kuacha kazi za ndani na kuanza kujishughulisha na biashara ndogondogo ya kuuza mboga kuanzia mwaka 2017.

"Nilianza biashara na mtaji wa Sh. 2000/- ambao unashindwa kukua kutokana na changamoto mbalimbali kwa sababu fedha ninayoipata kutokana na uuzaji wa mboga inatumika kulisha watoto, kulipia matibabu, kodi ya nyumba na wakati mwingine inaweza kufika mwezi nikawa sina hela ya kodi," anasema.

Biashara anayoifanya anasema inampatia Sh. 3,000 kwa siku ambazo ni kiasi ni kidogo mno.

Upendo anasema maisha ya familia yake yamekuwa magumu sana kwa sababu ameshindwa kumsaidia mwanae Alex kupata haki yake ya msingi ya kusoma kama walivyo watoto wengine.

"Changamoto niliyokuwa nayo sasa hivi, nikitoka nyumbani saa 9:00 usiku kwenda kununua mboga sokoni kwa ajili ya biashara inabidi nimfungie Alex ndani hadi nikirudi saa 12 asubuhi. Nikirudi nampikia chai na baadaye namfungia tena kuanzia saa 1:00 hadi saa 8:00 mchana nitakaporudi tena nyumbani," anasema

Mara nyingi Alex anashinda na njaa mpaka nirudi nyumbani ndipo anakula na kwamba kutokana na changamoto alizonazo ameshindwa kumtafutia mtoto wake shule maalumu kwa ajili ya watoto wenye ulemavu.

"Natamani sana mwanangu angepata shule asome kutokana na changamoto aliyonayo," Anasema

Anasema anatamani angepata msingi wa kufanya biashara akiwa karibu na watoto wake ili mtoto naye aweze kusoma.

"Mtoto anakosa hela ya kusoma kwa sababu sina uwezo, baba yake mtoto amenitelekeza kuanzia mwaka 2010 baada ya kuona mtoto ameanza kupata ulemavu, hajawahi kuja kumuangalia mtoto wake hadi leo." Anasema

"Mbali na hilo, sina ndugu wa kunisaidia, wazazi wangu wote walifariki.

"Ninachokumbuka mama yangu alifariki nikiwa mdogo sana ila baba yangu alifariki 2003 nikiwa darasa la saba na hadi sasa mimi nina miaka 30," anasema.

**HISIA ZAKE**

Baada ya mazungumzo Upendo anasema tatizo la kuwa na mtoto mlemavu ni mzigo kwake na anahisi ni muda wa kuwasilisha maombi kwa serikali na jamii impe msaada .

Kwanza anaomba familie zenye walemavu zikumbukwe na kusaidiwa akiomba wahisani wamsaidie kumnunulia sehemu ndogo hata kumjengea chumba kimoja ili aweze kuishi na watoto wake lakini pia apate mtaji kwa ajili ya kufanya biashara.

"Ninaomba wanininulie sehemu ndogo ya kujenga makazi kwa sababu hela ninayopata ni ndogo na inaishia kwenye nyumba ya kupanga ambayo haina umeme lakini pia namshukuru Mungu ingawa watoto wangu wamepata sehemu ya kulala," anasema na kuongeza kuwa kipato chake kinatoka kwenye kuuza mboga mitaani.

OMBI KWA SERIKALI

"Ninaiomba serikali kama inavyojenga shule za sekondari na msingi kwa kila kata ifikirie kuwajengea madarasa maalum kwenye shule hizo ziwe za msingi, za sekondari na hata vyuo watu wenye ulemavu.

Angalau ziwepo kwa kila shule ili nao waweze kusoma waondokane na adha ya kutokujua chochote kwenye elimu hasa wale wa familia maskini,"anasema Upendo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti na mwanzilishi wa Kikundi cha Wenye Ulemavu cha Umoja wa Kusaidiana Walemavu Chanika, Salma Ramadhani, anasema watoto wenye ulemavu wana changamoto nyingi sana hasa kama shuleni hawahudumiwi kama wanafunzi wengine wenye ukamilifu wa viungo.

Katika shule zinazojengwa nao wanatakiwa wawe na madarasa yao, ulemavu una utofauti, wawe na walimu maalumu na kama zinavyojengwa kwa kila kijiji au kata kuwapo madarasa maalumu ya walemavu katika maeneo hayo.

"Kwa mfano hapa Chanika ninapoishi kuna mtoto mwenye ulemavu akitaka kwenda shule inabidi mama yake ambebe ampeleke , amsimamie, usafiri shida hata kusomeshwa shida. Mkono na mguu vimepinda anahitaji msaada." Anasema

Anaeleza kuwa anahitaji msaada ana shida sana ni mtoto wa miaka 16 sasa hivi hivyo serikali iangalie namna ya kuwasaidia raia hao .


"Yaani namuonea huruma sana kwa sababu ana akili na anajua kusoma lakini kwenda shule hawezi mpaka dada yake au mama yake wambebe. Kila kitu anahitaji kubebwa, angepatiwa kitimwendo au baiskeli ya wenye ulemavu ingekuwa nafuu kwao. Tunaomba shule hizo ziwe na watu na vifaa vya kuwasaidia na kuwahudumia waliozidiwa na kuhitaji misaada." Anasema Salma.

"Sisi wenye ulemavu tunaomba serikali iwajengee madarasa maalum, iwape walimu maalum na vyoo maalumu ili kusaidia wanafunzi wenye ulemavu kuweza kusoma katika mazingira bora kama walivyo wanafunzi wengine." Anaongeza Salma.

Anaamini itakuwa ni suala la tija kama shule hizi zitajengwa pia katika kata ya Chanika kwa sababu watoto wenye ulemavu wapo wengi sana na pia wanaomba wapatiwe usafiri wao.

SAYANSI
NA MAGABILO
MASAMBU

# Ili kukabili msongamano masomo yawe kwa 'shifti'



Wanafunzi waklachiana nafasi darasani, inaweza kuwa njia ya kupunguza uwezekano wa kuambukizwa corona. **PICHA: MTANDAO**

JANA shule zimefunguliwa rasmi na imethibitishwa kwamba si wakati wa kuendelea kujifungia ndani 'lockdown' kwani kutasababisha matatizo mengi zaidi kwenye jamii. Ni kwa sababu uchumi wa mtu mmoja mmoja unategemea shughuli anazozifanya kila siku.

Kwa hiyo, kufungiwa kazi hizo kungeleta madhara makubwa kwa taifa.

Baada ya shule za msingi na sekondari kufunguliwa ni jambo jema kwa wanafunzi, wazazi, walimu pamoja na kwa serikali yenyewe inayoangalia uelekeo mpya wa corona.

Pamoja na tangazo hilo ni muda wa kuishauri serikali hasa Wizara ya Elimu, wakati wanafunzi wako madarasani kwani ni lazima waendelee kuwa salama zaidi kuepuka maambukizo ya COVID -19 kwasababu kipindi serikali ilipotangaza kufunguliwa shule ilieleza umuhimu wa kujihadhari.

Maana ya angalizo hilo ni kwamba ugonjwa upo ndiyo maana hadhari zinapaswa kuendelea kuchukuliwa na ili watoto wawe salama wakati wa masomo yao.

Shirika la Afya Duniani (WHO), pamoja na Wizara ya Afya zimeainishwa njia mbalimbali za kujikinga na ugonjwa wa corona, miongoni mwa njia hizo ni pamoja na kunawa mikono kila mara kwa maji tiririka na sabuni, kutumia vitakasa mikono venye asilimia zaidi ya 60 ya kileo, kuvaa barakoa na kukaa umbali wa zaidi ya mita mbili kutoka mtu hadi mtu.

> Ikimaanisha madarasa yatenganishwe mfano shule za msingi kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu. Hawa waingie asubuhi mpaka mchana na kisha waliosalia wanaingia mchana na kuendelea vivyohivyo kwa shule za sekondari ili kuwapa nafasi ya kupangwa kwa nafasi kwenye vyumba vya madarasa.

Hili nalo linaleta changamoto kwa vile hali halisi ya shule za nchi hii inafahamika kuwa ni finyu na uchache wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari ni dhahiri.

Wanafunzi wanakaa kwa kubanana kwani chumba kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 45 wanakaa zaidi ya 60 kwa shule nyingi, kwa hiyo uwezekano wa kuzingatia umbali wa angalau wa mita mmoja ni mgumu sana tena ikizingatiwa kwamba ugonjwa huu unasambaa haraka sana kwa kugusana ama kukaribiana na mwenye maambukizo.

### USHAURI

Ni katika maeneo mawili, moja ni kuhusu shule za kutwa za serikali na za binafsi, pili ni kuhusu shule za bweni pia za serikali na binafsi.

Kwa shule za kutwa ambazo wanafunzi wanakwenda kila siku shuleni na kurejea nyumbani jioni, kwahiyo ni wanafunzi ambao wana muingiliano mkubwa na jamii .

Wengi wanapokwenda shuleni wengine wanatumia usafiri kama daladala kwa mfano walioko Dar es Salaam au kwenye miji yenye misongamano mikubwa kunaweza kusababisha kupata maambukizo na kuyaleta shuleni ambako nako kuna msongamano kwenye vyumba vya madarasa na hivyo kufanya uwezekano mkubwa wa ikiwa mmoja amepata mahali fulani kusababisha wengi kuambukizwa.

### KUTUMIA AWAMU

Nini kifanyike sasa ? Kuna haja ya shule hizi zote za msingi na sekondari kuwa na shifti (kusoma kwa awamu mbili).

Ikimaanisha madarasa yatenganishwe mfano shule za msingi kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu.

Hawa waingie asubuhi mpaka mchana na kisha waliosalia wanaingia mchana na kuendelea vivyohivyo kwa shule za sekondari ili kuwapa nafasi ya kupangwa kwa nafasi kwenye vyumba vya madarasa.

Inawezekana ikawa usumbufu hasa namna ya kupanga ratiba za masomo kwa sababu madarasa yatagawanywagawanywa lakini sina hakika kama linaweza kuwa tatizo kubwa kwa walimu kufanya hivyo.

### MSONGAMANO WALIMU

Suala la awamu liende sambamba na kuwapanga kwenye shifti pia, kwasababu hali ya walimu ni ileile shule nyingi zinatumia madarasa kama ofisi kwa hiyo hata walimu nao wana misongamano kwenye ofsi zao.

Kwa upande wa shule za bweni huku kuchukua tahadhari kuna unafuu ikilinganishwa na shule za kutwa kwani hao hawajachanganyikana na jamii za watu wa nje ya shule licha ya kwamba kuna walimu wanaotoka nje ya mazingira ya bweni.

Wanafunzi wako bweni uwezekano wa kuzuia muingiliano na watu wa nje ni rahisi zaidi kwa watumishi kwa maana ya walimu na wafanyakazi wengine kuchukua tahadhari wao wenyewe ili wasiwe sababu ya maambukizo .

Wanaweza kutafuta mahitaji na kurudi shuleni lakini kwa wanafunzi hakuna shida wakishaingia wameingia na kutoka ni mwisho wa muhula kwa hiyo kama itatokea wamefika shuleni hakuna mwenye maambukizo si rahisi kuyapata.

Katika maelezo yake, Wizara ya Elimu ilieleza kwamba watoto wadogo chini ya miaka mitano wasivalishwe barakoa kutokana na maelekezo ya kitaalam ni jambo jema lakini watoto hawa wanatoka kwenye familia huku ambako sisi kama wazazi tunachangamana sana.

Kwa hiyo uwezekano wa kuwaambukiza watoto na wao wakapeleka shuleni ni mkubwa ndiyo maana njia sahihi ni shifti ili wakibaki wachache wanaweza kutawanywa vizuri kwenye vyumba na kuzuia kusongamana.

Kunawa mikono hilo litawezekana japo pia litakuwa na changamoto zake moja ikiwa ni upatikanaji wa maji ya kutosha ikizingatiwa kwamba kwasasa ni kipindi cha kiangazi hapo mbinu mbalimbali zitatumika ili kuhakikisha yanakuwapo na hapo kunahitajika ushirikiano mkubwa kati ya shule na wanavijiji au wananchi ili huduma za maji zipatikane pamoja na vitakasa mikono.

Pengine hili suala la shifti au awamu wizara ilishaliona na kulijadili.

Huenda ilionekana kuna kubwa lakini nashauri kama ilionekana litakuwa na changamoto ni bora zitafutiwe ufumbuzi ili lifanyike kwa nchi nzima na kama pengine hamkulijadili kama wizara ni wakati muafaka wa kulifanyia kazi.

Utaratibu huu unaweza kufanyika kwa majaribio mpaka mwezi Disemba 2020 kama utakuwa na mafanikio basi utaendelea mpaka pale hali itakaporidhisha kurudi kwenye utaratibu wa kawaida.

### KELELE ZA ADA

Aidha ni vyema kuzingatia ushauri wa serikali kwa wamiliki wa shule binafsi kuhusu malipo ya ada na michango mbalimbali kwamba busara inahitajika kati ya pande zote mbili kutokana na ukweli kuwa janga la corona limeathiri watu wengi kiuchumi.

Ajira nyingi zimekufa na mishahara kupungua na hivyo wapo wazazi watakaoshindwa kulipa ada za watoto wao kwa wakati, basi ni busara pia wamiliki na wakuu wa shule hizo kufahamu hilo ili kazi isiwe moja ya kudai ada kila wakati.

Badala yake ifahamike kwamba kuna tatizo la kiuchumi, kwa upande wa wazazi nao wajikongoje ili walimu nao wapate mshahara ili shughuli za uendeshaji wa shule zisiwe ngumu kiasi cha kukwama lakini ni muhimu zaidi busara na hekima ikatumika kabla ya kutazama upatikanaji wa fedha pekee.

***Maoni: 0689157789, magabilomjalifu@gmail.com***

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Likizo ya corona ilivyoliza watoto




Wakazi wakipita kwenye mitaa ya Mji Mkongwe, Unguja. **PICHA ZOTE : MTANDAO.**

WANAFUNZI wote Bara na Visiwani wameanza masomo jana baada ya kupumzika kwa miezi mitatu na nusu. Kwa wengi wawe wazazi, walezi, watoto na hata walimu kilikuwa kipindi kigumu.

Leo dunia inapokabiliwa na janga la corona na watoto kusimama kimasomo licha ya kwamba hapa nchini wamerudi shuleni, watoto waliotakiwa kulindwa wakiwa wametulia nyumbani kuanzia Machi hadi Juni 28, wapo mafisadi wa maadili waliotumia mwanya huo kuwadhalilisha.

Tangu Machi mwaka huu liliporipotiwa janga la corona na shule kufungwa watoto 10 wamedhalilishwa kijinsia Zanzibar na hizo ni rekodi za Chama cha Wanahabari Wanawake Zanzibar (Tamwa), ambao waliwapokea waathirika wakiomba msaada..

Licha ya takwimu hizo za kipindi hicho kifupi pia watoto 1,049 wamedhalilishwa Unguja na Pemba kwa miaka miwili kuanzia 2017 hadi 2019, ambao pia waliripoti Tamwa kwa kipindi hicho..

Mzuri Issa ,Mkurugenzi wa Chama cha Tamwa Zanzibar, anaeleza kusikitishwa na ongezeko la vitendo vya ubakaji watoto katika likizo ya corona, ambavyo baadhi ya watuhumiwa ni watoto wenyewe .

Anasema hiyo ni sehemu ndogo ya taarifa zilizofikishwa Tamwa na huenda hali ni mbaya zaidi, anataka jamii, wazazi, walezi na viongozi wa dini na vyombo vya sheria kusaidia kurekebisha tabia kwa watoto wa rika la miaka 16 ambao baadhi yao wanatuhumiwa kufanya makosa hayo.

Anaiomba serikali kuweka mipango madhubuti ya kubadilisha tabia ya vijana wa kiume ili kuruhusu wanawake na watoto kuishi kwa amani na kufikia malengo ya kimaisha.

Dokta Mzuri anaziomba mamlaka zinazohusika kuzishughulikia kesi hizo kwa haraka na kutoa adhabu zinazostahiki.

**KWANINI UNYANYASAJI**

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Zanzibar Dk.Sikujua Omar Hamdan, akizungumzia sababu za kuendelea vitendo vya watoto kudhalilishwa ikiwamo wazazi kumaliza kesi hizo mitaani na kushindwa kufika polisi na mahakamani anasema:

"Hufanya hivyo wakiwa na hofu ya kuona kwamba hawatasaidiwa, pamoja na kujua sheria.Wanabakia nyumbani na watoto wao. Hii inaonekana kwamba bado kuna mwamko mdogo wa kwenda kuripoti kesi polisi na mahakamani", anasema.

Hamdan anasema ushahidi bado ni tatizo na bado watu hawahudhurii mahakamani kutoa ushahidi jambo ambalo linapelekea kesi hizo kukosa hukumu.

Anakumbusha kuwa hakuna utaratibu mzuri wa kurikodi kesi hizo mahakamani na tafsiri ya sheria si makini kutokana na adhabu zinazotolewa zinaonekana kuwa hazistahiki.

"Kesi zilizoropitiwa mahakamani ni nyingi hivyo wadau wanatakiwa kukaa pamoja kwa ajili ya kuleta ufanisi vipi kesi za udhalilishaji zitafanyiwa mapitio",anashauri mhadhiri huyo.

Anaeleza kuwa kesi za ubakaji ndizo zinazoripotiwa kwa wingi mahakamani lakini hukumu zake haziridhishi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mahakama kukosa ushirikiano wa jamii hasa kutoa ushahidi.

**RUSHWA INAKWAMISHA**

Fatma Juma Mahmoud, Mkuu wa Dawati la Jinsia Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja, anasema kuwa jamii haijawa tayari kutoa ushahidi mahamakani na pia imetawaliwa na rushwa hali ambayo imepelekea kesi hizo kukosa hukumu.

"Lengo ni kuvitokomeza vitendo vya udhalilishaji hivyo cha muhimu ni utayari wa jami kutoa ushahidi mahakamani ili kuwasaidia watoto waliodhalilishwa",anasema.

Ofisa wa Wanawake na Watoto wa Wizara ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Muhamed Jabir, anasema kuna uwezekano kuwa majukumu ya baadhi ya wazazi yamepungua katika kipindi hiki cha corona hali ambayo imepelekea ongezeko la udhalilishaji.

Watoto wamepewa uhuru wa kupitiliza na kipindi hiki ambacho hawaendi shuleni wanazurura mitaani huku wazazi na walezi wakikwepa majukumu yao.

"Watoto wanahitaji uwangalizi mkubwa muda wote lakini licha ya shule kufungwa bado watoto wanazurura na kuwapa wadhalilishaji huitumia nafasi hiyo, "anaonya.




Mzuri Issa, Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar.

Cha kuzingatiwa ni kauli mbiu ya mwaka huu katika Siku ya Mtoto wa Afrika ni "upatikanaji wa mifumo ya haki iliyo rafiki kwa watoto wa Afrika".

Mwanaidi Ali Said , mratibu wa mradi wa kuimarisha familia ya kijiji cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (SOS) anasema katika kukumbuka vifo vya watoto hao wa Afrika wanaharakati wanatafakari na kuchukua hatua namna gani ya kushughulikia changamoto za watoto zikiwamo za elimu na haki nyingine.

Anasema siku hiyo hutumika kama ni sehemu ya kufanya ushawishi na utetezi wa kuimarisha uelewa wa mkataba wa Afrika kuhusu haki za watoto.

"Sisi wanaharakati tumeona ni muhimu kuangalia upatikanaji wa elimu kwa watoto katika kipindi hiki cha corona ikizingatiwa kuwa hivi sasa ni muda wa miezi mitatu shule zimefungwa kutokana na corona,"anasema.

Anaeleza kuwa kutokana na corona haki ya elimu kwa watoto imekosekana na baada ya ugonjwa huo kumeibuka mifumo mbalimbali ya kupata masomo ikiwamo ya kimtandao ambayo mengine si rafiki kwa watoto na imeathiri haki za watoto na maendeleo ya elimu.

Anasema kuna hatari zaidi ya baadhi ya watoto kutorudi tena shuleni baada ya kufunguliwa hasa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na watoto wengine kurudi nyuma kielimu.

**ATHARI KIMAZINGIRA**

Mkurugenzi wa taasisi ya Vijana (Zanzibar Youth Foram) Maulid Suleiman, anasema njia zozote zinazotumika ambazo hazijazoeleka kusoma na kufundisha zitakuwa si muafaka katika kutoa elimu.

Anaona kuwa utoaji wa elimu unategemewa kufanyika nyumbani unaonekana kuwa si muafaka kwa sababu sehemu ya kuwafundisha watoto masuala ya kitaalama.

"Licha ya kuwa kipindi hiki cha corona baadhi ya shule zimewaandalia wanafunzi masomo wakiwa nyumbani sio shule zote waliofanya hivyo,"anasema.

Aidha, anasema Wizara ya Elimu imeweka utaratibu wakutoa elimu kupitia vyombo vya habari lakini jamii haikuwa na muamko huo hivyo kiwango cha elimu miongoni mwa watoto kimeporomoka.

Mkurugenzi huyo anawataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao hivyo ni vyema kuwatayarisha na kuweka mazingira ya kufikia azma hiyo.

'Hivi sasa tumepata nafuu na maradhi yamepungua hivyo tunaimani kuwa shule zinavyofunguliwa watoto watapata elimu kama ilivyokusudiwa,"anasema.

**LIKIZO YA CORONA**

Baadhi ya wazazi waliozungumza na gazeti hili wanasema hivi sasa ufahamu wa watoto katika elimu umepungua na wameelekeza ufahamu wao katika michezo mbalimbali ikiwamo kuangalia 'game' kwenye simu na kompyuta, gololi, mpira wa miguu na rede kwa wasichana.

Safia Aboud ni mzazi wa watoto wawili, mkazi wa Unguja, anasema anawahimiza watoto wake kusoma lakini ufahamu wao umepungua.

Akizungumzia Wizara ya Elimu kuweka utaratibu wa kufundisha kwenye runinga , anaukosoa kuwa haujasaidia kwa sababu baadhi ya watoto hawana uelewa na pia hawakuandaliwa kujifunza kupitia TV na redio.

Hata hivyo, anaona kuwa hakuna kilichoharibika na kwamba tathmini ifanyike kufahamu mafanikio na changamoto za likizo ya corona.

## NA SABATO KASIKA

# Pale serikali ilipoelekeza wadau nao wafunguka

BAADA ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kukaa nyumbani kwa zaidi ya miezi mitatu ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, hatimaye wamerejea shuleni kuendelea na masomo.

Shule zilifunguliwa jana huku kukiwa na maelekezo maalum yaliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuhusu ulipaji ada ili asiwapo mwanafunzi atakayezuiwa kuanza masomo.

Wizara inaelekeza ada za shule zilipwe kulingana na makubaliano yaliyofikiwa mwanzoni mwa mwaka wa masomo na kwamba kusiwepo na nyongeza yoyote katika kiwango cha ada.

Katika sehemu ya maelekezo yake, wizara inataka wanafunzi wote wapelekwe shule kwa ajili ya kuendelea na masomo bila kikwazo chochote ili kukamilisha muhula na kusiwapo na nyongeza ya ada.

Aidha, wizara inasisitiza, wazazi wanapaswa kuzingatia kuwa kiwango cha ada kinakadiriwa kuzingatia gharama mbalimbali za uendeshaji wa shule, gharama ambazo ziliendelea kuwapo hata muda ambao shule zilikuwa zimefungwa, kama vile mishahara ya watumishi, ankara za umeme na maji na nyingine kadhaa.

Kutokana na maelekezo hayo ya serikali, baadhi ya wazazi wamekuwa na maoni tofauti walipozungumza na gazeti hili ambayo wanaamini yatakuwa na mchango wa kufanikisha watoto wao kusoma bila kuwapo malalamiko kwa pande zote mbili, yaani shule na wao.




Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako.

Deogratius David ni mkazi wa Morogoro, ambaye anasema, hatua hiyo ya serikali imesaidia kuwaondoa hofu baadhi ya wazazi ambao walidhani huenda watoto wao wakasimamishwa masomo.

"Pamoja na hayo, kila mzazi ambaye hajamaliza kulipa ada ya mtoto wake, afanye juu chini akamilishe, siyo kukaa kimya eti kwa sababu serikali imesema kusiwe na kikwazo," anasema David.

Anaongeza kuwa ni kweli corona imeyumbisha uchumi wa watu wengi, lakini pia ni muhimu kutambua kwamba, mishahara ya walimu na watumishi wengine wa shule binafsi na mahitaji mengine ya shule yanategemea ada zinazotolewa na wazazi.

"Maoni yangu ndiyo hao kwamba, bado wazazi tutimize wajibu wa kulipa ada, kwani katika maisha tunategemeana, yaani walimu wanategemea ada zetu na sisi tunawategemea watufundishie watoto wetu," anasema.

Naye Maua Bakari wa jijini Dar es Salaam, anasema, hatua ya wizara kutoa maelekezo itasaidia wanafunzi kusoma bila usumbufu na pia wazazi watapata muda wa kuhangaikia ada kwa nafasi.

Anasema, tangu serikali kutangaza kufungua shule, wazazi na walezi kila mmoja amekuwa na lake la kusema, kutokana na kwamba uingizaji wa kipato unatofautiana.

> "Ninashukuru kutoa maelekezo, ambayo ninaamini kwamba, kama yatazingatiwa, basi watoto wetu watasoma huku nasi tukijitahidi kutafuta ada na kuhakikisha tunalipa kwa

"Siyo siri, corona imesababisha biashara au shughuli za baadhi ya watu zimeyumba, zikiwamo zangu ambazo ni biashara ndogo na ninasomesha mtoto wangu katika shule binafsi," anasema Maua.

Anafafanua kuwa wiki iliyopita, alihudhuria kwenye mkutano ulioitishwa na uongozi wa shule kuzungumzia maandalizi ya kufungua shule ikiwamo pia kujadili malipo ya ada hasa baada watoto kukaa nyumbani miezi mitatu.

"Baadhi ya wazazi nikiwamo mimi, tuliomba uongozi wa shule uturuhusu kulipa ada kidogo kidogo kila mwezi badala ya kulipa ada kwa mkupuo, kwa sababu hatuna kitu," anasema.

Anasema, walijibiwa kuwa maombi yao yatafikiriwa kuona kama kuna uwezekano wa kufanya hivyo, na kwamba tangu wakati huo hawakupewa majibu hadi shule zimefunguliwa.

"Ninashukuru kutoa maelekezo, ambayo ninaamini kwamba, kama yatazingatiwa, basi watoto wetu watasoma huku nasi tukijitahidi kutafuta ada na kuhakikisha tunalipa kwa wakati,"anasema.

Kwa upande wake mkazi mwingine wa jijini Dar es Salaam aliyejitambulisha kwa jina la Pendo Ngaka anasema, mtoto wake anasoma darasa la kwanza na amepewa maelekezo kulipa kwa miezi yote mitatu ambayo alikuwa likizo.

"Maelekezo hayo yamenishangaza sana, kwani mtoto alikuwa hatumiwi kazi za nyumbani, sasa nitalipaji Sh. 300,000 wakati wakijua wazi kwamba hawakutoa kazi? Anahoji Pendo.

Anasema, kama walimu wa shule hiyo wamesikia maelekezo ya serikali na kuyazingatia, ana uhakika mtoto wake hatasumbuliwa na badala yake ataachwa aungane na wenzake kuendelea na masomo.

Mbali na hao, mzazi mwingine aliyezungumza na gazeti hili ni Jackson Nackson, ambaye anasema, mtu anapopeleka mtoto wake katika shule binafsi huwa ana uwezo wa kumudu gharama.

Hivyo, anaamini kila mzazi anayesomesha mtoto katika shule binafsi atamlipia ada, ila miezi yote mitatu ambayo watoto walikuwa nyumbani isihesabiwe na badala yake malipo ya ada yaanzie Julai.

"Lakini nisionekane kama niwaumiza wazazi wenzangu wanaosomesha watoto wao katika shule binafsi, bali nieleweke kuwa lengo langu ni kuwahimiza wasilalamike sana,"anasema Nackson.

Aidha, Nackson anawashauri wamiliki wa shule binafsi kutolazimisha wazazi kulipa ada kwa mkupuo, badala yake wawape nafasi na kupokea kile kidogo ambacho wazazi wanakipata ili wawe na nguvu ya kutafuta zaidi.

"Kwa nini ninashauri hivyo? Nina jirani yangu nilimsikia analalamika kwamba shuleni kwa mtoto wake wameambiwa walipe ada ya miezi sita kwa mkupuo badala ya mitatu wanalipa," anasema.

Anasema, shule zikisimamia hilo, zinaweza kusababisha baadhi ya watoto kubaki nyumbani kama serikali haitafuatilia maelekezo ambayo imeyatoa kwa wamiliki wa shule binafsi na kwa wazazi.

"Kutokana na mkanganyiko huo, ni vyema baada ya shule kufunguliwa, serikali izifuatilie ili kuona na kujua nini kinaendelea, ili kama kutakuwa bado kuna malalamiko, basi hatua za kuyatatua zichukuliwe," anasema.

Mkazi huyo wa jijini Dar es Salaam anasema, anaamini kwamba kila upande ukitumiza wajibu, watoto watasoma bila kuwapo malalamiko kutoka kwa wazazi, walezi na wamiliki wa shule.



# TAKUKURU yachunguza ubadhirifu mil. 124/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), jijini hapa imeanza uchunguzi wa ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 124 fedha za matazamio za Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), zilizolipwa kwa makandarasi isivyostahili.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkuu wa TAKUKURU jijini hapa, Sosthenes Kibwengo, alisema fedha hizo zililipwa isivyostahili na watumishi wasio waaminifu wa wakala wa Dodoma.

**Fedha hizo zililipwa isivyostahili na watumishi wasio waaminifu wa wakala wa Dodoma.**

Alisema TAKUKURU imeokoa Sh. milioni 44.5 kati ya fedha hizo zilizolipwa kwa makandarasi bila kustahili.

"Pamoja na kwamba uchunguzi unaendelea na hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa kwa wahusika, tunawataka wote waliosalia kurejesha fedha walizolipwa bila kustahili kabla ya mwisho wa mwezi huu," alisema.

Katika hatua nyingine, taasisi hiyo imebaini ukiukwaji wa taratibu za ununuzi pamoja na malipo yasiyoendana na kiasi halisi cha kazi kilichofanyika na kusababisha utekelezaji wa chini ya kiwango kwenye mradi wa maji Kijiji cha Songambele, Kongwa.

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) naye alifanya ukaguzi wa mradi huo ulioanza mwaka 2013 wenye thamani ya Sh. milioni 627.6 na kubaini upungufu kadhaa, tunaendelea na uchunguzi wake," alisema.

Alisema CAG alielekeza mambo kadhaa na ufuatiliaji umewezesha Halmashauri ya Kongwa kurejesha fedha za matazamio ya mradi huo Sh. milioni 32.2 kwenye akaunti ya amana ya halmashauri hiyo.

"Pia halmashauri hiyo imeilipa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Sh. milioni 12.5 zikiwa ni kodi ya zuio iliyotokana na malipo ya mkandarasi wa mradi huo Mwashinga Enterprises, ambazo awali zilichepushwa kwenye matumizi mengine," alisema.

## Serikali yaombwa kupaua madarasa Bwawani

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

SERIKALI imeombwa kupaua madarasa ya shule shikizi yaliyojengwa na wananchi wa kijiji cha Bwawani wilayani Chamwino, ili wanafunzi waondokane na adha ya kutembea umbali wa kilomita 10 kufuata elimu kijiji jirani.

Wakizungumza jana na Nipashe, wananchi hao walisema watoto wao wanatembea umbali huo kufuata elimu kijiji cha Gwandi.

"Hapa Bwawani ni kitongoji ambacho kipo pembezoni kwenye hii kata ya Zajilwa, watoto wanatembea umbali mrefu kila siku kwenda na kurudi tunaomba serikali ipaue haya madarasa ili wanafunzi wa chekechea wasome hapa karibu," alisema mkazi wa Bwawani, Mohamed Juma.

Alisema kutokana na tatizo la umbali, wakati mwingine huchangia asilimia kubwa utoro wa wanafunzi.

"Tuliamua kujichangisha na kujenga majengo ya shule ambayo yatatumika kama shule shikizi ambayo yatasaidia watoto wetu kuondokana na adha ya kutembea umbali huu kila siku," alisema.

Alisema pamoja na kuchangishana fedha na nguvu kazi zao, zaidi ya miaka minne sasa, madarasa hayo pamoja na ofisi za walimu hayajaezekwa na watoto wao kuendelea kutembea umbali mrefu kufuata shule mama.

"Hali hii imewafanya hata watoto wengine kuacha shule kwa kuwa mtoto wa miaka chini ya sita, hawezi kutembea kila siku mwendo huo wa kilomita zaidi ya 10 kwenda na kurudi kilomita 20, lazima tu aichukie shule," alisema Juma.

Naye, Martine Dahae, aliomba serikali kupaua majengo hayo ili watoto wapate haki ya kupata elimu kama ilivyo wa maeneo mengine nchini.

"Kama wameshindwa watuambie sisi tutafute njia ya kuezeka kama ambavyo tulijenga kwani ni miaka minne hatuoni lolote linalofanywa zaidi ya hili jengo tena kuanza kutumika kisiasa kwa watu kupigia kampeni za kutaka kuchaguliwa," alisema Dahae.

Kwa upande wake, Ramadhan Rashidi, alisema viongozi mbalimbali wa wilaya yao wameshafika katika eneo hilo na kushuhudia ujenzi wa majengo hayo, lakini kila wakienda wakiondoka hawarudi tena.

"Viongozi wa wilaya tayari walishakuja na kulikagua wakasema kuwa lipo vizuri kwani toka limejengwa miaka mnne iliyopita, mpaka leo hakuna hata ufa, na wao ndiyo walituambia kuwa tujenge na kupauwa watatusaidia, lakini mpaka sasa kimya na watoto wetu wanaendelea kupata shida," alisema Rashidi.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Dodoma, Mwalimu Amani Mfaume (kulia), akizungumza na wanafunzi kuhusu mipango mikakati waliyojiwekea kuhusu masomo na kujikinga na ugonjwa wa corona, baada ya shule kufunguliwa jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake KKKT wahamasisha wenzao fursa kugombea uongozi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAWAKE wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), wametakiwa kujitokeza kwa wingi kugombea udiwani na ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2020, ili kuongeza nafasi za wanawake kwenye ngazi za uamuzi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Wanawake wa kanisa hilo, Shile Sheshu, alipokuwa akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Wajane wa kanisa hilo, jijini Dodoma.

Sheshu aliwataka kuchangamkia fursa hiyo ili kuongeza idadi ya wanawake kwenye ngazi za uamuzi na kuleta usawa wa kijinsia.

Aliwaomba kufanya maombi kwa ajili ya kuombea uchaguzi huo ili ufanyike kwa haki na amani.

"Tuna jukumu la kuomba na kufunga kwa ajili ya uchaguzi huu ili ufanyike kwa huru, haki na amani pia ni haki yenu kujitokeza kugombea badala ya kuishia kwenye maombi tu," alisema.

Aliwahimiza kujitokeza kwa wingi kupiga kura na kuchagua viongozi watakaowatumikia Watanzania bila kujali itikadi za vyama vyao.

"Pia wajane tuendelee kumuunga mkono Rais John Magufuli amefanya juhudi kubwa kwa ajili ya Watanzania wanyonge, pia niwaombe msikate tamaa pamoja na changamoto nyingi tulizonazo, endeleeni kufanya kazi kwa bidii ili kumuunga mkono Rais wetu," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Wajane wa kanisa hilo, Ester Kiranga, aliomba serikali na asasi za kiraia kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaojitokeza kuwanyima haki za kimsingi wajane kupitia mali walizozipata wakati waume zao wakiwa hai.

Aliomba serikali na asasi za kiraia zishirikiane kwa pamoja ili wajane wapate haki zao za kimsingi bila kudhulumiwa wala manyanyaso.

Pia, alisema kumekuwapo na unyanyasaji mkubwa wa kutopewa haki wajane wanapoondokewa na wenza wao.

"Hapa nchini Tanzania kuna zaidi ya wajane 500,000 na wengi wao wanaishi katika dimbwi la umaskini na uonevu mkubwa kutokana na kutotendewa haki kama walivyokuwa wakitarajia," alisema.





# TARI yaanza kukabiliana na udumavu mazao lishe

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Uyole, iliyopo mkoani Mbeya imeanza kusaidia kulipunguza tatizo la udumavu hapa nchini kwa kuzalisha mbegu za maharage lishe, mahindi lishe na viazi lishe ambazo zina uwezo wa kukabiliana na tatizo hilo linalowakumba hasa watoto.

**Pamoja na mkakati huo wa kupunguza udumavu, lakini TARI Uyole imeendelea na uzalishaji wa mbegu za teknolojia ya kisasa zenye kuongeza tija.**

Akizungumza katika mahojiano maalumu na gazeti hili, Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema uzalishaji wa mazao hayo yenye viini lishe umeshaanza na kupokelewa na wakulima wengi hasa wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema TARI Uyole imeamua kuja na mkakati wa kuzalisha mbegu zenye viini lishe kwa kutumia mazao hayo kutokana na kuwapo kwa udumavu nchini, hivyo kupitia vyakula, hivyo ambavyo vinapendwa kuliwa na Watanzania wengi wanaamini tatizo hilo sasa litapungua kwa kiwango kikubwa.

Dk. Bucheyeki, alisema pamoja na mkakati huo wa kupunguza udumavu, lakini TARI Uyole imeendelea na uzalishaji wa mbegu za teknolojia ya kisasa zenye kuongeza tija na visumbufu ambazo zinahitajika kama malighafi za uchumi wa viwanda.

Mratibu wa kitaifa wa zao la maharage wa TARI Uyole, Dk. Rose Mongi, alisema wanafanya utafiti wa mbegu za maharage za aina mbalimbali ikiwamo zenye viini lishe na tayari wameshatoa mbegu aina 42 tangu utafiti ulivyoanza.

Alisema kuwa miongoni mwa mbegu hizo pia zipo wanazoweza kutumia bila shaka yoyote watu wenye matatizo ya vidonda vya tumbo kutokana na utaalamu unaotumika kwenye utafiti wa mbegu hizo na wengi ambao walikuwa wakishindwa kula maharage kwa sasa wanatumia.

Dk. Mongi, alisema mkakati wa sasa wanaoendelea nao ni pamoja na kuendelea kufanya majaribio ya mbegu hizo ili ziweze kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo imeanza kujitokeza kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni ili mbegu hizo ziweze kwenda na mabadiliko hayo.

Naye Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa kituo hicho, Dk. Ndabhemeye Mlengera, alisema kilimo cha maharage na mazao mengine kama mahindi pia kinatumia teknolojia ya kilimo hifadhi ambacho kinazingatia misingi ya kutosumbua udongo na kufunika ardhi hasa kipindi hiki cha mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kilimo hifadhi kwa kipindi cha msimu huo kimesaidia kuongeza uzalishaji kutokana na kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuwafanya wadudu rafiki wa kwenye udongo wanaosaidia kuozesha masalia ya mazao kuendelea kufanya vizuri kutokana na kuwa na mazingira rafiki.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kulia), akiwakabidhi watendaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, vifaa kwa ajili ya kuendeshea Mahakama Mtandao, hivi karibuni, ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kuharakisha uendeshaji wa kesi na kupunguza mahabusu magerezani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Chunya kinara kuzalisha tumbaku bora

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WILAYA ya Chunya mkoani Mbeya imetajwa kuwa ndiyo inayozalisha tumbaku bora kuliko maeneo yote nchini kutokana na wakulima wengi kufuata kanuni za kilimo bora cha zao hilo.

Hayo yalisemwa na Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Stanley Mnonzya, wakati wa uzinduzi wa masoko ya tumbaku nchini uliofanyika kitaifa katika Kata ya Lupatingatinga wilayani Chunya.

Alisema mikoa inayozalisha tumbaku nchini ni 12, lakini katika maeneo mengine wakulima hawafuati maelekezo ya wataalamu wa zao hilo hali ambayo inapunguza ubora, hivyo akawataka viongozi wa vyama vikuu vya ushirika kutoa elimu kwa wakulima wao.

"Mkoa wa kitumbaku wa Chunya unazalisha tumbaku bora sana, ni vyema mikoa mingine ikaja kujifunza huku ili tuzalishe tumbaku inayofanana kwa ubora katika maeneo yote," alisema Mnonzya.

Alisema pamoja na ubora huo, lakini kuna tatizo la baadhi ya wakulima kushindwa kufuata sheria za kilimo cha zao hilo ikiwamo kuwatumikisha watoto kwenye mashamba na kutopanda miti ya kukaushia zao hilo.

Alisema hali hiyo inasababisha baadhi ya wanunuzi wa zao hilo kujitoa, na kwamba ili kudhibiti hali hiyo, TTB imeanza kuwaondoa kwenye daftari la usajili wakulima wanaobainika kukiuka taratibu hizo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alisema pamoja na kwamba wilaya yake inasifika kwa uzalishaji wa tumbaku bora, lakini mwaka huu ubora huo umepungua kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema mwaka huu kulikuwa na mvua nyingi kupita kiasi hali ambayo ilisababisha wakulima kushindwa kukausha zao hilo kwa ubora unaotakiwa.

"Tatizo lingine linalowakabili wakulima wetu ni bei kuwa chini kutokana na kuwa na mnunuzi mmoja ambaye hana ushindani wowote, tunaiomba wizara itusaidie kutufuta wanunuzi wengine," alisema Mahundi.

Kwa upande wake Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema baadhi ya wanunuzi wa zao hilo walikimbia soko la Tanzania na kukimbilia Zimbabwe, Malawi na mataifa mengine kutokana na matatizo mbalimbali yaliyojitokeza nchini kuanzia mwaka 2014.

Alisema kwa sasa baadhi ya matatizo hayo yametatuliwa na serikali na tayari wizara inaendelea na mazungumzo ya kibiashara na mataifa ya Misri na China ili yaje kununua tumbaku inayozalishwa nchini.

"Wachina walisema wako tayari kuja kununua, lakini kwa masharti kuwa tuzalishe mbegu ya tumbaku wanayoitaka wao na walituletea tumeifanyia majaribio kule Kahama, lisingekuwa janga la corona wangekuwa wameshakuja sasa tunasubiri hali itulie," alisema Hasunga.

# Serikali yakabidhi X-ray kwa Hospitali ya Rufani Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeikabidhi Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya mashine ya kisasa ya miozi (X-ray) ambayo inadaiwa kuwa itaongeza ufanisi kwenye matibabu kwa maelezo kuwa iliyokuwapo ni ya muda mrefu na ni mbovu.

Mashine hiyo ilikabidhiwa kwa uongozi wa hospitali hiyo na Mhandisi Onesmo Haule, ambaye aliifunga katika kitengo cha mionzi cha hospitali hiyo na kuwaelekeza watumishi wa kitengo hicho namna ya kuitumia kwa ufanisi.

Akipokea mashine hiyo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Gloria Mbwile, aliishukuru serikali kwa kuikumbuka hospitali hiyo kwa maelezo kuwa mashine waliyokuwa wanaitumia ina zaidi ya miaka 20 na hivyo ilikuwa imechakaa.

Alisema mashine hiyo itasaidia kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kwa maelezo kuwa ina uwezo wa kutoa majibu kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

"Tunaishukuru sana serikali hasa Wizara ya Afya chini ya Waziri Ummy Mwalimu na wasaidizi wake, mashine tuliyokuwa nayo hapa ina umri wa mtu mzima... ilikuwa imechoka na hata ufanisi wake ulikuwa mdogo, lakini hii tunaamini itatusaidia sana kuboresha huduma," alisema Dk. Gloria.

Alisema watahakikisha wanaitunza vizuri mashine hiyo kwa kuifanyia matengenezo ya mara kwa mara ili idumu kwa muda mrefu zaidi, huku akiwataka watendaji wa kitengo hicho cha mionzi kuhakikisha wanawapatia wananchi huduma bora.

Dk. Gloria alisema mashine hiyo inaifanya hospitali hiyo kuondokana na vifaa vya analojia na kuingia kwenye mfumo wa matumizi ya vifaa vya kidigitali.

Akikabidhi mashine hiyo kwa niaba ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhandisi Haule aliwataka watendaji wa hospitali hiyo kuitunza mashine hiyo na kuitumia kwa usahihi ili itumike kwa muda mrefu.

Bila kutaja bei halisi ya mashine hiyo, alisema ni miongoni mwa vifaa vinavyouzwa kwa bei kubwa, hivyo ikiharibika inahitaji fedha nyingi kwenye matengenezo.

# Wafanyakazi wa hoteli waomba kurudishwa kazini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wafanyakazi wa hotelini visiwani hapa wamedai kuwa licha ya serikali kuruhusu shughuli zote kurejea baada ya kupungua kwa janga la corona bado hawajaruhusiwa kurudi kazini.

Wakizungumza na Nipashe, walisema kuwa tangu kuingia kwa janga la corona wamepewa likizo bila ya malipo na hakuna kiwango chochote cha fedha wanachopatiwa.

Wahid Khamis, ambaye ni miongoni mwa wafanyakazi hao aliiomba Wizara ya Kazi kuhakikisha wanarejeshwa kazini ili waendelee kufanya kazi na kupata kipato.

"Kwa kweli corona tunaambiwa imeisha, lakini bado hali za kiuchumi ni ngumu maana kazini tumepewa likizo bila malipo wala hatujui likizo hiyo itaisha lini," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Vijana (Zanzibar Youth Forum), Maulid Suleiman, aliitaka Serikali ya Zanzibar kuwasaidia vijana waliowekeza katika sekta ya utalii ambao kwa sasa hawana ajira kufuatia kujitokeza kwa athari za ugonjwa wa corona na hoteli kushindwa kupokea wageni kwa zaidi ya miezi minne sasa.

Alisema sekta ya utalii imeathirika vibaya na ugonjwa wa corona na vijana waliowekeza katika sekta hiyo ikiwamo wafanyakazi wa hoteli, wasambazaji wa vyakula hotelini na watembezaji wa wageni wamepoteza ajira kwa zaidi ya miezi minne sasa.

Alisema licha ya serikali kuruhusu kuanza kwa sekta ya utalii kwa kuingia kwa wageni nchini, bado hali haijawa nzuri kutokana na nchi zingine za Ulaya ugonjwa wa corona upo.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Mkunazini Zanzibar, Dk. Michael Hafidh, alisema tayari wameanza maandalizi ya kupokea wageni na watalii wanaozuru kanisa hilo baada ya shughuli hizo kufungwa kwa zaidi ya miezi minne kutokana na janga hilo.

Alisema zaidi ya vijana 20 wamekosa kazi katika kipindi cha miezi minne ya kufungwa kwa shughuli za kutembeza watalii katika eneo la kanisa la Mkunazini Unguja na kuathirika kiuchumi.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Mohamed Abdalla, alisema tayari serikali imeruhusu kuanza kwa shughuli za utalii kwa ndege kubwa kuja moja kwa moja kutoka Ulaya.

"Matarajio yetu makubwa kuona shughuli za huduma za utalii zinarudi kama kawaida kwa ndege kubwa kuanza safari zake...najuwa itachukua muda kidogo kwa sababu wenzetu Ulaya ugonjwa bado upo," alisema.

# Kidato cha 6 watakiwa kuepuka udanganyifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi wa kidato cha sita walioanza Mtihani wa Taifa jana, kuepuka udanganyifu wa aina yoyote wanapokuwa katika mitihani hiyo.

Akizungumza na wanafunzi hao katika shule mbalimbali za sekondari Mjini Unguja, alisema kujiamini wakati wa kufanya mitihani ndio njia pekee itakayowasaidia kujibu vyema mitihani yao na kupata ufaulu wa daraja la juu.

**Lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia Wizara ya Elimu kuondosha kabisa zero na kupunguza alama za daraja la nne...**


Pembe aliwataka wanafunzi kuhakikisha wanasoma maelezo ya mtihani unavyoelekeza vizuri kabla ya kujibu maswali, ili waandike majibu ya uhakika na ufasaha.

Alisema lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia Wizara ya Elimu kuondosha kabisa zero na kupunguza alama za daraja la nne ili Taifa lizalishe wataalamu mbalimbali nchini.

Kwa upande wake mwalimu msimamizi wa mitihani katika Shule ya Dk. Ali Mohamed Shein iliyopo Mwembeladu, Meja mstaafu Zagu Haji Zagu, alimpongeza Waziri wa Elimu kwa utaratibu aliojiwekea kuhakikisha anapita katika shule kuhamasisha wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yao, hali itakayowapa moyo wa kufanya vizuri.

Naye mwanafunzi Amne Pembe Ali, kwa niaba ya wanafunzi wenziwe, alimhakikishia Waziri Pembe kuwa pamoja na kupitia wakati mgumu wa kufungwa shule kutokana na maradhi ya Covid -19, watafanya vizuri katika mitihani yao na kufaulu daraja la kwanza.

Katika ziara hiyo waziri huyo alikagua Shule ya Lumumba, Jang'ombe, Haile Sselassie, Hamamni na Kiponda, jumla ya wanafunzi 2,686 wa kidato cha sita visiwani hapa wameanza mitihani yao jana.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akizungumza na wanafunzi wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari ya Lumumba na Jang'ombe, kabla ya kuanza Mitihani yao ya Taifa jana. **PICHA: RAHMA SULEIMA**

# Wanafunzi wa kike vyuo vikuu waonywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), imewataka wanafunzi wa kike wa vyuo vikuu kuacha tamaa na kushughulikia masomo yao ili taifa liweze kuwa na wataalamu wa kike.

Mkurugenzi wa jumuiya hiyo, Jamila Mahmoud, aliyasema hayo wakati akizungumza na wanafunzi wanawake wa vyuo vikuu Zanzibar kuhusu masuala ya jinsia.

Alisema baadhi ya wanafunzi wa kike hushindwa kumaliza masomo yao kutokana na kujiingiza katika mambo maovu kwa kutaka vitu ambavyo hawana uwezo navyo.

"Wapo baadhi ya wanafunzi wanabeba ujauzito wakiwa vyuoni, wengine hupata ujauzito kutokana na tamaa kwa kutaka vitu vya thamani ambavyo hawana uwezo navyo," alisema.

Aliwataka wanafunzi hao kutoa elimu ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanafunzi wenzao ili wanapofanyiwa vitendo hivyo waripoti sehemu husika na kufanyiwa kazi.

Alidai baadhi ya wanafunzi wa kiume na walimu huwadai rushwa ya ngono wanafunzi wa kike kwa kisingizio cha kuwasaidia masomo ili waepukane na matokeo mabaya.

Naye Rufea Khamis Juma, Ofisa Miradi kutoka ZAFELA, alisema wameamua kuwapa elimu ya udhalilishaji wanafunzi hao ili kujua athari zake na kuepukana na vitendo hivyo.

Kwa upande wao wanafunzi hao wa vyuo vikuu, walisema mafunzo hayo watayafanyia kazi na kuwafikishia wanafunzi wenzao ili kuepukana na vitendo hivyo vinavyoweza kuwaharibia masomo yao.

Mwanafunzi Mariyam Mbarouk, alisema kuna mambo ambayo yanaweza kutumika kupunguza au kuondoa vitendo vya udhalilishaji ikiwamo sheria kufanyiwa kazi ipasavyo ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wadhalilishaji.

# Viongozi 4 CCM mbaroni kwa tuhuma za rushwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Arusha, inawashikilia wajumbe wanne viongozi wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa huo, kwa tuhuma ya kutoa rushwa ili wateuliwe kugombea ubunge.

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha, James Ruge, aliwataja wajumbe hao, ni Sifaeli Pallangyo Mjumbe wa Baraza la Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Upendo Ndorosi Katibu wa Walezi Wilaya ya Longido na Laraposho Laizer, Katibu wa Wazazi Wilaya ya Longido na Mjumbe wa Baraza la Wazazi Mkoa wa Arusha na Godwait Mungure, Katibu wa Jumuiya hiyo Wilaya ya Meru.

Alisema Juni 26 mwaka huu TAKUKURU ilipokea taarifa kwa raia mwema kuwa Lilian Ntiro, anayetarajiwa kugombea ubunge kwa tiketi ya wazazi Mkoa wa Arusha, alimpatia Sifaeli Pallangyo, fedha kwa ajili ya kwenda kuwahonga wajumbe wilayani Longido.

Taarifa hiyo, ilisema baada ya TAKUKURU kupokea taarifa hiyo, walishirikiana na maofisa wa taasisi hiyo, Wilaya ya Longido, kuandaa mtego na walifanikiwa kuwakamata watuhumiwa wanne kila mmoja na kiasi chake cha fedha zikiwa zimeandaliwa kwa ajili ya kuwapa wajumbe wa Longido.

Taarifa hiyo, ilisema Pallangyo, alikamatwa na Sh.140,000, Upendo Malulu, Sh. 552,000, pamoja na simu iliyoonyesha mawasiliano na watuhumiwa wenzake.

Watuhumiwa wengine ni Laraposho Laizer, alikamatwa Sh.117,000 pamoja na ikiwa na mawasiliano na watuhumiwa wenzake.

Mwingine ni Godwait Mungure, Katibu wa Wazazi Kata ya Kikatiti ambaye alikuwa na simu ndogo ikiwa na mawasiliano na mtuhumiwa mwingine, Sifaeli Pallangyo.

## Vijana Songwe waonyeshwa fursa biashara, uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** SONGWE

TAASISI ya Sekta Binafsi nchini (TPSF) imewataka vijana mkoani Songwe kutumia vizuri fursa za kibiashara na uwekezaji zilizosheheni mkoani humo, ili kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbaye, aliwaambia vijana wakati wa Kongamano la Fursa za Kibiashara kwa Vijana wa Mkoa wa Songwe kuwa fursa zilizomo mkoani humo ziweza kubadilisha maisha yao kuwa bora zaidi kiuchumi endapo watazitumia ipasavyo.

"Kongamano la Kijana na Ndoto yako ni njia mojawapo ya kuwaunganisha vijana na fursa zilizopo hapa Songwe ikiwamo kilimo, utalii, afya, madini na namna ambavyo Songwe inavyoweza kutumia nafasi yake kama lango kuu la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)," alisema Simbeye.

Akizungumza katika kongamano hilo mwisho mwa wiki mkoani Songwe, Simbeye aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Songwe chini ya Brigedia Jenerali mstaafu Nicodemus Mwangela kwa kushirikiana kwa karibu na TPSF katika kushughulikia changamoto za vijana ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali za kibiashara na uwekezaji.

Alisema TPSF kwa kuungwa mkono na wadau mbalimbali kama Taasisi ya Trademark East Africa (TMEA) wamefanikisha mashaurino baina ya sekta za umma na binafsi(Public-Private Dialogues).

"TPSF tumefurahishwa sana jinsi sekta za umma na binafsi zinavyoshirikiana katika kushughulikia changamoto zilizopo kwenye jamii hususani vijana. Tunaamini kongamano hili litawajengea vijana ari ya kujiamini na maamuzi sahihi pamoja na kuwaunganisha na fursa lukuki zilizopo mkoani Songwe," alisema.

Mkuu Mkoa huo, Brigedia Mwangela aliwataka vijana kuendelea kutumia fursa zilizopo, ubunifu pamoja na muda wao vizuri ili kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii mkoani humo.

Kijana Charles Mkemesa ambaye pia alikuwa mshiriki alisema Kongamano hilo limempa fursa kujua mambo mengi na kumjengea uelewa mpana wa fursa zilizopo mkoani Songwe tofauti na awali.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtambani, Wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, wakifurahia maji baada ya kuzinduliwa kwa kisima shuleni hapo jana, kilichojengwa kwa ushirikiano wa Taasisi ya Time To Help na Shule za Feza za jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## H'shauri Dar zatakiwa kujifunza Kinondoni

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI za Mkoa wa Dar es Salaam zimetakiwa kuiga mfano wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani, Serikali Kuu pamoja na wadau kama ilivyotekelezwa katika Manispaa ya Kinondoni.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, wakati akihitimisha ziara yake ya siku mbili wilayani Kinondoni kukagua na kukabidhi miradi kwa kamati ya siasa ya jijini humo.

Alisema kila halmashauri jijini humo inakusanya mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali na wanapaswa kuacha alama kupitia shughuli za maendeleo.

"Kinondoni nawapongeza sana mmefanya kazi inayoonekana na kuacha alama kwa wananchi, kipindi cha nyuma haya mambo hayakuwapo licha ya kwamba Manispaa zilikuwa zinakusanya," alisema Makonda.

Kuhusu mradi wa soko la kisasa la Magomeni, alisema lililojengwa kwa fedha za Serikali Kuu, na kwamba ni chanzo kikubwa cha mapato katika manispaa hiyo, na limewezesha mazingira mazuri ya biashara kwa wafanyabiashara.

Awali, Mkuu wa Wilaya hiyo, Danieli Chongolo, alisema wilaya hiyo imekamilisha miradi kwa wakati na inakabidhiwa kwa kamati hiyo, na kwamba wataendelea na utekelezaji wa miradi mingine.

## Makamu Mwenyekiti CUF Z'bar asimamishwa

**Na Boniface Gideon**

BARAZA Kuu la Uongozi Taifa la Chama cha Wananchi (CUF) limemsimamisha uongozi Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Abbas Juma Muhunzi, kwa tuhuma za kukiuka maadili ya uongozi.

Maamuzi hayo yamefikiwa katika kikao kilichofanyika mwishoni mwa wiki kwa siku tatu mfululizo, ambapo Baraza Kuu la Uongozi la CUF lilijadili makosa yaliyowasilishwa na wajumbe dhidi ya Makamu Mwenyekiti huyo.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi, Mahusiano ya Umma wa CUF, Mohamed Ngulangwa, alisema walifanya uamuzi huo kwa kuzingatia ibara za 83(1) (b) na 94(1) zinazolipa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa mamlaka ya muongozo katika kushughulikia masuala ya kinidhamu kwa viongozi wakuu.

Alisema baada ya wajumbe kupokea tuhuma dhidi ya Muhunzi na kufanya mjadala wa kina, baraza hilo lilitoa nafasi kwa mlalamikiwa kujitetea, alikiri kufanya makosa yaliyoelekezwa kwake na akakiachia kikao kuamua dhidi yake.

# Serikali DRC yakumbwa na mvutano mkubwa

**KINSHASA,** DRC

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) inaendelea kukumbwa na malumbano ya ndani baada ya mtafaruku kati ya vigogo kutoka pande mbili zilizoko madarakani.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa hakuna kinachoendelea kati ya pande mbili zilizoko madarakani, muungano wa vyama wa FCC unaoongozwa na Joseph Kabila, na muungano wa CACH wa Rais Félix Tshisekedi (pichani chini), bali ni mvutano, hali ambayo imezua mkanganyiko.

Baadhi ya watu wa karibu na serikali ya DRC wanasema chanzo ni mapendekezo matatu yaliyoletwa na wabunge wawili kutoka Chama cha FCC, Sakata na Minaku.

Mapendekezo ya muswada wa sheria kuhusu mageuzi ya vyombo vya sheria ambayo hayakuungwa mkono na wengi.

Wabunge hao wanashuku kwa baadhi ya mapendekezo yaliyotetewa na wabunge hao wawili, nia ya kurasimisha mfumo wa mahakama kwa serikali kwa ujumla na kwa Waziri wa Sheria upande mwingine.

Ledjely, mmoja wa wachambuzi wa masuala ya kisiasa kutoka Guinea akihojiwa katika moja ya kituo cha habari alisema ni hatua ya Waziri wa Sheria kuwasilisha mtazamo wa serikali unaohusiana na mapendekezo hayo matatu kwa Bunge, bila kumhusisha Rais Félix Tshisekedi au serikali.

Alisema hatua hiyo Rais Tshisekedi anafasiri kama kudharau mamlaka yake. Kitendo ambacho kilimkasirisha hadi kuchukuwa uamuzi wa kusitisha ghafla ushiriki wake katika kikao cha Baraza la Mawaziri ambacho alikuwa anaongoza siku ya Ijumaa wiki iliyopita.

Alisema siku iliyofuata mambo yalishika kasi baada ya kukamatwa na Naibu Waziri Mkuu, Célestin Tunda Ya Kasende, chini ya shinikizo.

Mwendesha mashtaka aliamua kumwachilia waziri huyo baada ya mahojiano ya muda mfupi.

Hali hiyo imeendelea kuzua hali ya sintofahamu nchini DRC na tayari pande hizo mbili zimeendelea kuzusha sintofahamu nchini humo. **RFI**



# China yatumia mitishamba kutibu ugonjwa wa corona

**BEIJING,** China

WAKATI wanasayansi duniani wakipambana kutengeneza chanjo ya virusi vya corona, China ambayo imekuwa kinara katika utengenezaji wa dawa za asili imetengeneza dawa ya asili inayojulikana kama 'Traditional Chinese Medicine (TCM)' ili kutibu ugonjwa wa corona.

Gazeti moja lilizinduliwa na serikali ya China lilidai kuwa asilimia 92 ya wagonjwa wa corona wa nchi hiyo walitibiwa na dawa hiyo.

TCM ni dawa ya zamani ambayo imetengenezwa kwa kutumia mitishamba. Dawa hiyo ni maarufu sana nchini China licha ya kwamba ilizua mjadala kuhusu matumizi yake mtandaoni.

Wataalamu wanasema China inajaribu kuisambaza dawa hiyo ndani ya nchi na nje ya nchi, lakini wataalamu wa afya bado hawaamini uwezo wake wa kutibu.

**Kuna watu wengi ambao wanapenda dawa hiyo tangu enzi za mababu na kuiita kuwa hazina ya watu wa China.**

Wizara ya Afya ya China imeweka kitengo maalum cha TCM pamoja na mwongozo wa kukabiliana na virusi vya corona, wakati Televisheni ya Taifa ilidai kuwa dawa hiyo ilifanya kazi vizuri katika mlipuko wa miaka ya nyuma kama Sars mwaka 2003.

Kuna dawa sita ambazo zimekuwa zikitangazwa kutibu virusi vya corona, dawa mbili ambazo ni maarufu moja ni 'Lianhua Qingwen' - ambayo ni mchanganyiko wa dawa za mitishamba 13 kama vile Forsythia na Rhodiola rose - na Jinhua Qinggan ambazo zilizinduliwa mwaka 2009 katika mplipuko wa H1N1.

Dawa hiyo ilitengenezwa na mchanganyiko wa vitu 12 vikiwamo asali, majani ya 'mint' na mizizi ya mmea wa 'liquorice'.

Wanaounga mkono dawa ya TCM wanadai kuwa hakuna madhara yoyote ukitumia dawa hizo, lakini wanasayansi wanasema ni muhimu kwa vipimo vya kisayansi kufanyika ili kuhakikisha usalama wa dawa hiyo.

Taasisi ya Afya Marekani ilisema labda dawa hiyo itasaidia kuondoa dalili, lakini suala la kutibu corona bado kuna mashaka.

Aidha, dawa ya TCM inazidi kupata umaarufu nchini China na inaonekana kuna hitaji kubwa la kimataifa. Baraza la Taifa la China, mwaka jana lilikadiria kuwa kiwanda cha TCM kitakuwa na thamani ya dola bilioni 420 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2020.

Rais wa China, Xi Jiping, alisema kuna watu wengi ambao wanapenda dawa hiyo tangu enzi za mababu na kuiita kuwa hazina ya watu wa China. **BBC**



Askari wa Jeshi la Pakistan wakiimarisha ulinzi nje ya soko la hisa baada ya magaidi kuvamia. **PICHA: REUTERS**

# Magaidi washambulia soko la hisa

**KARACHI,** Pakistan

WATU wasiopungua 10 wakiwamo magaidi wanne wameuawa katika shambulio dhidi ya soko la hisa la Pakistan, lililoko katika mji wa bandari wa Karachi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi wa kanda, Sharjeel Kharal, aliviambia vyombo vya habari kwamba walinzi wanne wa usalama, ofisa mmoja wa polisi na raia mmoja ni miongoni mwa waliouawa.

Alisema magaidi wote wanne wameuawa na kwamba watu wengine saba, wakiwamo askari polisi watatu wamejeruhiwa katika shambulio hilo.

Mkurungenzi Mtendaji wa soko la Hisa la Pakistan, Farrukh Khan, alisema shambulio hilo lilikuwa zito, lakini kwa bahati nzuri magaidi hawakuweza kuingia eneo kuu la jengo la soko hilo.

Zaidi ya wafanyabiashara na wafanyakazi 1,000 waliokuwapo katika jengo wakati wa shambulio kwa mujibu wa ripoti.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa washambuliaji hao walivamia eneo hilo la soko la hisa baada ya kurusha bomu la mkono kwenye lango kuu la jengo, lakini maofisa wanasema kuwa walishindwa kufika kwenye ghorofa ya biashara ya soko la hisa.

Wafanyakazi waliokuwa ndani ya jengo walijifungia kwenye vyumba na wengi wao wakaokolewa.

Wanamgambo kutoka kundi la Baloch Liberation Army wamekiri kutekeleza shambulio hilo.

Makundi ya Baloch yamekuwa yakipigana kwa muda mrefu yakidai kujitenga na kutaka kuwa na mgao mkubwa wa rasilimali katika Jimbo la Balochistan.

Pakistan imekuwa ikivamiwa na wanamgambo wa Kiislamu, lakini mashambulizi kama haya yamekuwa nadra sana miaka ya hivi karibuni.

Shambulio la Jumatatu lilianza pale wanamgambo wenye silaha walio na bunduki waliporusha bomu la mkono na kuanza kufyatua risasi eneo la usalama nje ya jengo la soko la hisa.

"Walikuja kwa kutumia gari la Corolla rangi ya fedha na wakasimamishwa na polisi nje ya lango kuu, ambapo ufyatulianaji wa risasi ulianza," alisema Mkuu wa Polisi wa Sindh, Ghulam Nabi Memon.

Walinzi walijibu shambulio hilo na kuwaua wavamizi wote wanne waliokuwa wamejihami kwa silaha. **DW**

# ZIDANE: 'ASISTI' YA BENZEMA NI BORA KWA MSIMU



**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anaamini kiwango alichokionyesha Karim Benzema kwa pasi yake ya mwisho wakati Real Madrid ikiibuka na ushindi dhidi ya Espanyol ni bora zaidi kwa msimu huu.

Benzema alimtengenezea pasi murua Casemiro ambaye aliiwezesha Madrid kuibuka na ushindi wa 1-0 na kuwapeleka pointi mbili zaidi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Jumapili.

Fowadi huyo alitoa pasi ya mwisho kwa kisigino na mpira kipita katikati ya miguu ya mlinzi, Bernardo Espinosa na Casemiro akaisukumizia golini kiurahisi.

Na kocha wa Madrid, Zidane hakushangazwa na hilo na anaamini pasi hiyo ya mwisho ya Benzema inaweza kuwa bora zaidi kwa msimu huu.

"Wala haikunishangaza mimi. Ni mchezaji ambaye anatengeneza vitu," amesema akiliambia gazeti la AS.

"Na Casemiro yuko pale. Inaweza kuwa bora zaidi kwa msimu huu."

Bao hilo liliinyanyua Madrid kwa pointi mbili zaidi kileleni dhidi ya wapinzani wao Barcelona, huku zikiwa zimebakia mechi sita LaLiga kumalizika.

Zidane amesema anatarajia mbio za kuwania ubingwa zitakwenda hadi siku ya mwisho ya msimu huu.

"Mechi sita zimebaki na hii itaamuliwa siku ya mwisho. Unatakiwa kupambana kila mechi," alisema.

## Kocha Newcastle atamba kumsajili De Bruyne

**NEWCASTLE,** England

NEWCASTLE United ilitolewa kwenye michuano ya kombe la FA na Manchester City Jumapili, lakini kocha wake, Steve Bruce alikipenda kile alichokiona.

Kevin De Bruyne ndiye aliyekuwa na mchango mkubwa kwa ushindi huo wa City wa mabao 2-0 pale kwenye dimba la St James' Park, akianza kufunga la uongozi kwa mkwaju wa penalti katika kipindi cha kwanza baada ya Fabian Schar kumfanyia faulo Gabriel Jesus.

Goli lile liliwaonyesha njia ya kwenda kwenye robo fainali na Raheem Sterling akawahakikishia safari hiyo baada ya Dwight Gayle kushindwa kutumia nafasi aliyoipata kusawazisha.

Hivyo, nahodha wa zamani wa Manchester United, Bruce alikunwa na kiwango cha De Bruyne, ambaye pia alifunga bao la kuvutia kwa City wakati walipokutana kwenye mchezo wa Ligi Kuu Novemba mwaka jana, na alitania Newcastle inaweza kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

Akimzungumzia De Bruyne mara baada ya mchezo huo, bosi huyo wa Newcastle, Bruce alisema: "Atabakia hapa.

"Atabakia hapa, na hii ni mpya kabisa kwa Newcastle usiku huu. Ameshafanya ya kutosha Manchester City na sasa anakuja hapa na kuichezea Newcastle."






## Werner: Ilikuwa lazima Chelsea

**DORTMUND,** Ujerumani

TIMO Werner amesema alilazimika "kuumiza upande mmoja" baada ya kuamua kuondoka RB Leipzig kujiunga na klabu yake mpya ya Chelsea.

Werner kesho Jumatano atakamilisha usajili wake kule Chelsea kwa ada ya euro milioni 53 kutoka kwa miamba hao wa Ujerumani.

Fowadi huyo wa Ujerumani mchezo wake wa mwisho kwa Leipzig Jumamosi iliyopita alifunga mabao mawili wakati wakiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Augsburg na kuwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo.

Na Werner ameelezea uamuzi wake wa kuitenga Leipzig, huku vijana hao wa kocha, Julian Nagelsmann wakiwa tayari wamefuzu kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya mlipuko wa virusi vya corona kwa kuwatupa nje Tottenham Hotspur.

"Bila shaka inaniumiza mimi, kwamba ziwezi kuwasaidia (RB Leipzig) kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini mimi ni mchezaji wa Chelsea FC kuanzia Julai Mosi," alisema Werner akiiambia Sportbuzzer.

"Ilikuwa wazi kabisa pande zote mbili - Chelsea, RB na upande wangu - tulitakiwa kulimaliza hili. Bila shaka nilijaribu kuwa nje ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kadili ninavyoweza na ilikuwa wazi kwamba lazima niuumize upande mmoja.

"Hatimaye wakala wangu alikubaliana na klabu zote mbili."

Werner alifunga mabao manne katika mechi nane kuisaidia Leipzig kufuzu kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambayo imepangwa kumaliziwa jijini Lisbon nchini Ureno kwa mtoano wa mechi moja moja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alimaliza msimu wa Bundesliga akiwa na mabao 28 katika mechi 34 alizocheza msimu huu.

## HABARI MICHEZO

# Arteta: Pepe sasa anaelewa anachofanya

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anaamini Nicolas Pepe "ana nafasi kubwa", baada ya tayari kuelewa nini anachotakiwa kufanya pale Arsenal.

Mchezaji huyo aliyesajili kwa bei iliyoweka rekodi klabuni hapo kutoka Lille alifunga bao la ufunguzi kwenye ushindi wa robo fainali ya kombe la FA dhidi ya Sheffield United Jumapili, akifunga kwa mkwaju wa penalti kipindi cha kwanza.

Pepe sasa amefunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho tangu aanze kuichezea klabu hiyo, na Arteta anaamini kuna mengi bado yanakuja kutoka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25

"Nimehamasika kuhusu kile alichokileta kwa timu msimu huu," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya ushindi wa 2-1 pale kwenye dimba la Bramall Lane huku la pili likifungwa na Dani Ceballos.

"Nafikiri anajua na kuelewa nini anahitaji kufanya wakati ambao akiwa hana mpira.

"Nimefurahi sana leo. Ukiangalia namna alivyokuwa akicheza na kujilinda, inavutia kwa kile anachokifanya na ni mbunifu.

"Ni aina ya mchezaji tunayemhitaji. Mara zote haitabiriki nini kinaweza kutokea wakati akiwa na mpira.

"Nafikiri anakwenda kwenye njia sahihi kabisa."

Pepe alijiunga na Arsenal wakati Unai Emery akiwa kocha, na Arteta ameonesha kuvutiwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast baada ya kuchukua mikoba ya kukinoa kikosi hicho cha pale kwenye dimba la Emirates mwishoni mwa mwaka 2019.







# INTER YAKARIBIA KUMSAJILI HAKIMI

**MILAN,** Italia

INTER Milan imefikia hatua nzuri kwenye majadiliano juu ya mpango wa kumsajili Achraf Hakimi kutoka Real Madrid, Ofisa Mtendaji wa Nerazzurri hao, Beppe Marotta, amethibitisha.

Hakimi amekuwa nyota pale Borussia Dortmund msimu huu, akiwa amejiunga kwa mkopo wa miaka miwili kutoka kwa miamba wa LaLiga, Madrid mwaka 2018.

Hata hivyo, Dortmund ilithibitisha Jumamosi kwamba, Hakimi hatabakia kwa mkataba wa kudumu, huku Thomas Meunier tayari akiwa amenunuliwa kwenye kikosi hicho cha kocha, Lucien Favre.

Sasa, Hakimi anapanga kuhamia Inter, huku Marotta akithibitisha ripoti hiyo kwamba wanakaribia kufikia makubaliano, na Mkurugenzi wa michezo, Piero Ausilio ndiye anayeshughulikia dili hilo kwa klabu hiyo ya Serie A.

"Tumefikia pazuri kwenye majadiliano na tutaona nini kitatokea ndani ya siku chache zijazo," alisema Marotta akiiambia Sky Italia.

"Nataka kuwa na heshima kubwa kwa wachezaji wote wanaocheza na kujituma kwa timu. Na tunaangalia majaliwa ya baadae kwa kusajili wachezaji wengine.

"Ni hatua nzuri na muhimu kwa timu. Lazima nisema Ausilio amefanya kazi nzuri sana. Sasa tunatakiwa kumaliza kila kitu, lakini Ausilio amefanya kila kitu kwa siku zilizopita kwa kipindi cha miezi miwili."

Hakimi ambaye ni mlinzi wa kimataifa wa Morocco mwenye umri wa miaka 21, alifunga mabao tisa kwenye mashindano yote aliyoichezea Dortmund msimu huu 2019-20.

# *Kalou afikia pazuri kutua Botafogo*

**RIO DE JAINERO,** Brazil

SALOMON Kalou anakaribia kukamilisha usajili wa kwenda Botafogo, kwa mujibu wa mmoja wa wajumbe wa kamati ya Utendaji ya klabu hiyo ya nchini Brazil.

Fowadi huyo wa zamani wa Chelsea, Kalou, atakuwa huru bila mkataba pale Hertha Berlin kuanzia leo Julai Mosi na mazungumzo na yupo kwenye mazungumzo na miamba hao kutoka jiji la Rio de Janeiro. Botafogo, ambao wana mchezaji wa zamani wa Milan, Keisuke Honda kwenye vitabu vyao, walishindwa kukamilisha mpango wa kumsajili Yaya Toure, ambaye mgombea wa urais wa Vasco da Gama, Leven Siano ameahidi kumsajili.

Hata hivyo, matumaini yao ni kumpata mchezaji mwingine wa zamani wa Ivory Coast na mpango huo unaweza kukamilika hivi karibuni.

"Tayari ana mkataba wa awali, lakini alitaka maelezo zaidi ju ya mkataba wake na tumemtumia," Mjumbe huyo wa kamati tendaji ya Botafogo, Carlos Augusto Montenegro aliiambia SporTV.


"Nafikiri ipo sawa. Na kama mgombea wa urais wa Vasco hatatokea, pengine atakuja."

Kalou, alisimamishwa na Hertha Mei kwa sababu ya kuvunja kanuni za kujilinda na maambukizi ya virusi vya corona.

Botafogo imeripotiwa kumpa ofa ya miezi 18 mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye klabu kadhaa za Ulaya pia zimeonesha nia ya kumtaka.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AJIANDAA KUWA KOCHA BARCELONA

## Aelezea mipango ya kuirudisha Barca kwenye njia za...

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amesema anajindaa "sana" kuwa kocha wa Barcelona wakati miamba hao wa Camp Nou wakiangalia uwezekano wa kurudi kwake.

**Kocha huyo wa Al-Sadd, Xavi alihusishwa na na fasi ya Barca mapema mwaka huu wakati mabingwa hao wa LaLiga walipomfukuza Ernesto Valverde, kabla ya kumchukua Quique Setien Januari.**

Barca imekuwa kwenye kiwango kisichovutia msimu huu - huku bingwa huyo mtetezi akiwa amepitwa pointi mbili kileleni na wapinzani wao Real Madrid kwenye mbio za kuwania ubingwa wa LaLiga huku zikiwa zimebakia mechi sita. Huku akielezea mipango yake kwa Barca, Xavi mwenye umri wa miaka 40 alisisitiza hatakwenda pale hadi apate uzoefu wa kutosha wa kufanya uamuzi.

"Matumaini makubwa niliyonayo sasa ni kuwa kocha wa Barca na kuirudisha Barca kwenye njia zake za ushindi," alisema Xavi, ambaye ameiongoza Al-Sadd kubeba taji la Qatari Super na kombe la Qatar, akiiambia Sport.

"Sio mimi bali ni wachezaji hawa na ushindi wa Barca. Na kwa namna yoyote, jambo hili linawahusu watu wa benchi la ufundi ambao wanajiandaa kwa hili na kufanya vitu viwe vya kuvutia."

Xavi, ambaye alishinda mataji 25 kwa kipindi chake cha uchezaji pale Barca, aliongeza: "Mimi ni mtu wa klabu. Nataka kurudi kwa wakati sahihi kuanza mradi kutokea sifuri kabisa.

"Nimesema hivyo mara nyingi tu, lakini nataka kuchukua uamuzi wa kisoka pale Barcelona.

"Ni wazi kwamba, baada ya uchaguzi kila kitu kitakuwa sawa, bila shaka yoyote siwezi kuondoa uwezekano.

"Walikuja kwangu Januari, tulikuwa tunazungumza. Niliwaambia matokeo yake na muda utakavyokuwa."

## ZISIKUPITE

### LIVER YAMWANIA KOULIBALY

LIVERPOOL ipo mbele ya Manchester City kwenye mbio za kumuwania mlinzi wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, kwa kutoa ofa ya mlinzi wao wa Croatia, Dejan Lovren mwenye umri wa miaka 30, kama sehemu ya uhamisho. ***(Tuttosport)***

### HAKIMI NI SUALA LA MUDA

OFISA Mtendaji wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amesema klabu yake imefikia hatika hatua nzuri ya majadiliano ya kumsajili, Achraf Hakimi mwenye umri wa miaka 21 ambaye anacheza kwa mkopo kule Borussia Dortmund. ***(Goal)***

### SANCHEZ KUONGEZEA MKATABA

KLABU ya Inter Milan ina mipango ya kumuongezea muda kuendelea kucheza kwa mkopo hapo fowadi wa Manchester United na Chile, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 31, lakini mazungumzo yanaonekana kuwa magumu. ***(Sky Sports Italy, via Mirror)***

### YAPATA NGUVU KWA ONANA

CHELSEA wameongezewa nguvu na kocha wa Ajax, Erik ten Hag juu ya mipango yao ya kumsajili mlinzi wa kimataifa wa Argentina, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 27 na golikipa wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 24, ambapo amesema wanaweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Express)***

### MAN CITY KUMSAJILI MORENO

MANCHESTER City inapanga kumsajili fowadi wa Juventus na Hispania, Pablo Moreno mwenye umri wa miaka 18, katika dili ambalo litamhusisha winga wa Ureno, Felix Correia, mwenye umri wa 19. ***(Goal)***

### ARTHUR ASAINI MIAKA 5 JUVE

KIUNGO wa Barcelona na Brazil, Arthur mwenye umri wa miaka 23, amesaini mkataba wa miaka mitano kujiunga na Juventus kwa ada ya pauni milioni 72.5, huku kiungo wa kimataifa wa Bosnia and Herzegovina, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 30, akielekea upande mwingine kwa ada inayotajwa kuwa pauni milioni 60. ***(Sky Sports)***

### GREALISH ANUKIA MAN UNITED

NAHODHA wa Aston Villa, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kuhamia Manchester United baada ya kununua nyumba Kaskazini Magharibi mwa England. ***(Express)***

### INTER KUMUUZA SKRINIAR

INTER Milan inafikiria kumuuza mlinzi wa Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, kipindi hiki cha majira ya joto, huku Manchester City ni miongoni mwa klabu zilizoonesha nia ya kumtaka. Fowadi wa City na Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, anaweza kutumika kwenye dili hilo. ***(Calciomercato)***

### BENFICA YAMTAJA POCHETTINO

KLABU ya Benfica inaonesha nia ya kutaka kumteua kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino kama kocha wao mpya. Pochettino mwenye umri wa miaka 48 hana kazi tangu Novemba, mwaka jana. ***(Record)***

HABARI MICHEZO

## Prisons, Simba mapato kiduchu

**Na Somoe Ng'itu,** MBEYA

MECHI ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Maafande wa Prisons dhidi ya mabingwa wa ligi hiyo msimu wa 2019/20, Simba kutoka jijini Dar es Salaam imeingiza kiasi cha Sh. milioni 31, imeelezwa.

Mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini hapa ilimalizika kwa sare ya bila kufungana ambayo ilitosha kuwapa ubingwa Wekundu wa Msimbazi ambao walikuwa wanahitaji pointi moja tu.

Mapato hayo ni kidogo ukilinganisha na kiasi cha Sh. milioni 58 kilichopatikana kwenye mchezo uliopita katika Uwanja huo wakati Mbeya City wakiwakaribisha mabingwa hao.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Mbeya (MREFA), Elias Mwanjala, alisema idadi chache ya mashabiki kuingia uwanjani ilitokana na tamko la awali la kuufungia uwanja huo lililotolewa na serikali siku moja baada ya mchezo kati ya Mbeya City dhidi ya Simba.

Mwanjala alisema MREFA kwa kushirikiana na wamiliki wa uwanja wataendelea kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kupambana na kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona.

Alisema pia walilazimika kupandisha kiingilio cha chini katika eneo la mzunguko kutoka Sh. 5,000 ambacho kimezoeleka kwa wadau wa mchezo huo na kuwa Sh. 7,000 ili kupunguza mashabiki.

## Makocha, viongozi waipongeza Simba

**Na Adam Fungamwango**

MAKOCHA na viongozi mbalimbali nchini na nje ya nchi, wameipongeza klabu ya Simba kwa kutwaa ubingwa wa soka Tanzania Bara kwa msimu wa 2019/20, ikiwa ni kwa mara ya tatu mfululizo.

Makocha na viongozi hao wamesema kuwa ubingwa wa Simba hautokani tu na kikosi kizuri walichonacho, lakini mipango, matunzo na uwekezaji wa klabu hiyo.

Kocha wa Prisons, Mohamed Rishard Adolf, ameipongeza Simba na kusema kuwa ilikuwa na kikosi kizuri, chenye wachezaji wazuri waliokamilika kila idara, lakini uongozi wao pamoja na uwekezaji ambao umefanyika ndani ya klabu hiyo ndiyo unaowafanya kuwa na ubora huo.

"Tunashukuru kwa sare tulioipata, tulitaka pointi tatu, lakini tumepata moja, tumebakisha mechi sita, tunajua huko mbele nini tutafanya," alisema kocha huyo baada ya kikosi chake kutoka sare ya bila kufungana kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya.

Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars, Bakari Shime naye pia ameipongeza klabu ya Simba na kusema kuwa timu hiyo ilistahili kuwa mabingwa kutokana na kuonekana kama vile haikuwa na upinzani wa kutosha kutoka kwa timu zingine.

Msemaji wa Yanga, Hassan Bumbili alisema kuwa anawapongeza Simba, lakini wao kama Yanga wanachofanya kwa sasa ni kutengeneza kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao na hawana uhakika wanachukua kama ligi ikiendeshwa kwa haki.

# AJIBU, MIRAJI WAFUNGUKA KUBEBA KOMBE LIGI KUU

**Na Somoe Ng'itu,** MBEYA

WACHEZAJI Ibrahim Ajibu na Miraji Athumani 'Sheva' wamefurahi kunyakua taji la kwanza la Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na Simba maarufu Wekundu wa Msimbazi.

**Nyota hao walianza kucheza kandanda katika klabu hiyo kwenye timu ya vijana (Simba B), na baadaye kuondoka, Ajibu akisajiliwa kwa watani zao, Yanga huku Sheva akienda kuitumikia Lipuli FC ya mkoani Iringa.**

Akizungumza na gazeti hili baada ya kumalizika kwa mechi kati ya Tanzania Prisons dhidi ya Simba, Ajibu, alisema anamshukuru Mungu kwa kufanikiwa kushinda taji hilo msimu huu baada ya kurudi "nyumbani".

Ajibu alisema Simba ndio timu iliyomkuza katika mchezo huo, na mafanikio ambayo ameyapata msimu huu akiwa na klabu hiyo kwake ni faraja kubwa.

"Niliondoka kwa heshima na nimerudi kwa heshima mahali nilipokuzwa, nimefanikiwa kutimiza ndoto zangu kwa kutwaa taji la heshima la Ligi Kuu, asanteni mashabiki wa Simba, Simba Nguvu Moja," alisema Ajibu.

Sheva alisema ndoto yake kubwa ilikuwa kushinda taji hilo na baada ya kurejea Msimbazi aliamini ndoto zake zitatimia.

Mshambuliaji huyo alisema baada ya kutwaa taji hilo sasa akili yao ni kukamilisha mechi za ligi zilizopakia kwa mafanikio na baadaye kuhamishia nguvu kwenye michuano ya kimataifa.

"Ni jambo la furaha kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, ilikuwa ni ndoto yangu ya muda mrefu, niliamini itatimia msimu huu baada ya kurejea Simba, tunawashukuru wote tuliopambana tangu mwanzo wa msimu," alisema Sheva.

Simba ilifanikiwa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara juzi baada ya kufikisha pointi 79, ambazo hazifikiwi na timu nyingine, ambazo kila moja imebakiza mechi sita mkononi.



Msanii wa sarakasi Ally Shayo akifanya vitu vyake kwenye onyesho la bendi ya Waluguru Original, mjini Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

## *Kocha Prisons aeleza mechi iliwakataa*

**Na Somoe Ng'itu,** MBEYA

BAADA ya timu yake kulazimisha sare ya bila kufungana na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Kocha Mkuu wa Prisons, Mohammed Rishard 'Adolf' amesema kikosi chake hakikuwa na bahati katika mchezo huo wa juzi.

Adolf aliliambia gazeti hili washambuliaji wake hawakuwa makini kwa kashindwa kufunga zaidi ya mara nne wakiwa wamebaki na kipa wa Simba, Aishi Manula.

Hata hivyo, kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kwa kutokata tamaa na kuendelea kuisumbua safu ya ulinzi ya mabingwa hao mara tatu mfululizo.

"Hatukutumia vema nafasi tulizopata, nimekuwa nikiendelea kulifanyia kazi tatizo hili la mshambuliaji wangu mara kwa mara, lakini tukumbuke tulikuwa tunacheza na timu bora, timu yenye wachezaji wakubwa na wenye kujua nini wanataka," alisema kocha huyo.

Nahodha wa Tanzania Prisons katika mchezo huo, Benjamin Asukile, alisema timu yao ilistahili kupata ushindi katika mchezo huo kama wangekuwa makini zaidi.

Asukile alilalamika pia mwamuzi, Aboubakar Mturo, kutoka Mtwara kuwanyima penalti baada ya beki wa Simba kuunawa mpira ndani ya eneo la 18.

"Tunamshukuru Mungu tumemaliza mechi salama, wao wamekuwa mabingwa, lakini sisi pia tumelinda heshima yetu, hawajatufunga katika mechi zote mbili tulizokutana," Asukile alisema.

Prisons ambayo juzi ilifikisha pointi 43, itaendelea kubakia nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Sokoine kuwakaribisha Polisi Tanzania katika mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa Julai 4, mwaka huu.

Michezo
Jumanne Juni 30, 2020
Nipashe



Xavi ajiandaa kuwa kocha Barca UKURASA 22



Mshambuliaji wa Boma FC, Gaudence Mwaikimba (kulia), akiwania mpira na wachezaji wa Pan African, katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza uliochezwa Uwanja wa Uhuru. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga, Kagera mechi ya kisasi

● ● ● Yanga itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha mabao 3-0...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema wanahitaji kulipa kisasi katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Kagera Sugar inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

**Yanga itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha mabao 3-0, walichopata mara ya mwisho wakipokutana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Eymael alisema anaandaa kikosi cha ushindi na anaamini wako tayari kulipa kisasa kwa kuwaondoa Kagera Sugar katika mashindano hayo.

Eymael alisema hataki kupoteza mechi hiyo na hawako tayari kumbukumbu ya kichapo kutoka kwa timu hiyo ijirudie katika mchezo huo ambao utawasaidia kuendelea na safari ya kusaka nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Alisema anawaheshimu Kagera Sugar ni timu yenye wachezaji wazuri na wataingia uwanjani kupambana kutafuta matokeo chanya katika mchezo wao huo utakaokuwa wa ushindani kwa pande zote.

"Hii ni mechi ngumu sana kwa pande zote mbili, binafsi tunahitaji kulipa kisasi pia kuhitaji kucheza nusu fainali ili tuje kucheza fainali ya FA michuano ya FA ndio itatuongoza kushiriki michuano ya kimataifa, tuko makini," alisema Eymael.

Kocha huyo pia aliipongeza Simba kwa kutetea ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo na kueleza kikosi hicho kilistahili kutwaa kombe hilo.

"Simba, Kagera wameonyesha mpira mzuri wa wachezaji kucheza vizuri, tofauti na mechi zetu za hivi karibuni, nina kazi katika mchezo dhidi ya wapinzani wetu wa FA, kwani waliwahi kutusumbua," alisema Eymael.

Mechi nyingine ya robo fainali ya michuano hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Sahare Stars dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

## ZFF yatoa mchanganuo wa fedha

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar, ZFF, limetoa mchanganuo wa fedha shilingi milioni 21 zilizotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein.

Fedha hizo lengo lake ni kuzisaidia timu za Ligi Kuu ya Zanzibar wakati huu zinarudi kwenye ligi.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahamada Vuai, amesema kila timu ya Ligi Kuu imepewa shilingi milioni moja kwa ajili ya maandalizi ya timu.

Alisema mbali na fedha hizo ambazo klabu zimesaidiwa, lakini pia zimepewa nauli kwa timu ambazo zinaenda kucheza kutoka kituo kimoja kwenda kingine (Unguja na Pemba), pamoja na sehemu ya chakula kwa timu ambazo zitakaa kituo kimoja kwa muda mrefu.

"Hapa itakuwa kwa timu wageni, kwa mfano timu ya kituo cha Pemba itakapokuja katika kituo cha Unguja, serikali watatoa chakula kwa kipindi ambacho watakuwapo hapo, na timu ya kituo cha Unguja itapokwenda Pemba itakuwa hivyo hivyo," alisema Vuai.

Aidha, alisema hadi sasa ratiba ya ligi hiyo haijibadilika na inatarajiwa kuanza Julai Mosi kama ilivyopangwa na shirikisho hilo kupitia Kamati ya Mashindano na Bodi ya Ligi.

Hata hivyo, ameendelea kuzisisitiza klabu kufuata miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Afya katika kujikinga na virusi vya corona.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042